SHAABAN ROBERT



# Mapenzi Bora

SHAABAN ROBERT

# MAPENZI BORA

*Copyright © 1958 by SHAABAN ROBERT*

*First edition*

*This book was professionally typeset on Reedsy.*
*Find out more at reedsy.com*

*MAPENZI BORA*

*SHAABAN ROBERT*

*1958*

# Contents


| | |
|---|---|
| UTANGULIZI | 1 |
| MAPENZI BORA | 3 |
| KIELELEZO | 116 |

# UTANGULIZI

KUSUDI la kitabu hiki ni kuandalia mahitaji ya watu waliofikia fahamu ya kuwaza na kuhoji neno au kitu au tendo kwa akili, ingawa haitakuwa vibaya kama kitasomwa na watu wo wote ambao hawajafikia upeo kama huo wakipenda kujiweka tayari kwa zamu yao.

Watu ambao wana dhana ya kuwa mapenzi si kitu cha maana, waonywa katika kurasa hizi kuwa wanapatwa na hasara kubwa kwa kupitwa bila ya kujua na uzuri na fahari, heshima na utukufu ambao hustahili kuwa wao wenyewe. Wana miliki ya majo-hari ambayo hawajui thamani yake.

Baadhi ya watu hudai kuwa mapenzi karaha kuzungumzwa. Watu kama hawa hawachekeshi kidogo. Kiswahili si lugha ya watoto na vitabu vya chuoni tu. Huweza kuzungumza biashara na dini kama kiwezavyo kuzungumza sheria na mapenzi. Halali zilizomo katika mapenzi hushinda halali zilizomo katika sheria yo yote iliyopata kutengenezwa na mwanadamu. Karaha kuzungumza kitu kilicho halali na adili katika mafundisho ya wanadamu! Mzaha gani huu?

Wale wasemao kwamba mapenzi karaha hawawa-funzi wazazi kukaa vema na watoto wao, wala watoto kuwa wema na amini kwa wazazi wao. Hawawafunzi watu wajibu wa kutegemeana katika dunia. Huharibu umoja na ujirani, uaminifu

na urafiki kwa fikira zao za upuzi. Mungu hupenda watu. Stahili ya watu si kumchukia yeye.

Mapenzi ni jambo moja katika mambo yaliyo muhimu na wajibu kwa mtu katika maisha yake. Atakupenda nani katika dunia kama hutayari kupenda wengine wala kuheshimu mapenzi yao? Jambo lililo muhimu na wajibu kama hili huwa huru kuzungumzwa na mtu ye yote atakae kufanya hivyo.

Neno lisilokuwa la wajibu kwa watu ndilo neno la kudharauliwa, si mapenzi.

Waaidha, kama pana dhana ya kuwa *mapenzi* ni neno lisilo maana njema katika kamusi za lugha hii, sina budi kusema kwamba kamusi hizo si sahihi kama zita-zamiwavyo kuwa, na zisipotupiwa macho zikatengene-zwa upesi zitaudhi wanunuzi kwa kuonyesha dharau kubwa katika matumizi ya lugha.

**SHAABAN ROBERT**

***Tanga***

***Tanganyika territory***

***April 5, 1958***

# MAPENZI BORA

1
JINA limetakadamu,
Na moyo umeazimu,
Kabla juma kutimu,
Kuandika simulizi.
2
Pindi nikiwa mzima,
Muda ukipata juma,
Tawapa habari nzima,
Nikijaliwa pumzi.
3
Nikifunguliwa heri,
Na nguvu ya kufikiri,
Nitatunga kwa shairi,
Wimbo tunu nchi hizi.
4
Hata kama siku hizi,
Mwili wangu una ganzi,
Kabla robo ya mwezi,
Makala yatabarizi
5

Yatabarizi makala,
Kwa uwezo wake allah,
Apaye watu chakula,
Uzima na usingizi.
6
Toka kalamu kushika,
Arobaini miaka,
Bado sijapumzika,
Na kuiacha siwezi.
7
Kutunga na kutangua,
Kuwaza na kushangaa,
Sijakoma robo saa,
Kila siku nina kazi.
8
Kwa wino na karatasi
Kusoma na kudurusi,
Macho yangu nayahisi
Kuona yana tatizi.
9
Kuona natatizika,
Kwa nuru kunitoweka,
Na kila nikiandika,
Herufi huwa si wazi.
10
Macho yamejaa kiwi,
Herufi hayatambui,
Walakini kazi hii,
Kuiacha sifanyizi.
11
Japo dhaifu wa mwili,

Napenda kutawakali,
Kazi hii ya asili,
Na kuitupa siwezi.
12
Na kuacha sikubali,
Siwezi kwa kila hali,
Kila asili ni mali,
Kuacha haipendezi.
13
Kuitupa neon gumu,
Na kama litalazimu,
Tadhuriwa na mizimu
Ninazo fikira hizi.
14
Jadi itanisumbua,
Nijutie kuzaliwa,
Hapa katika dunia,
Maisha yatanihizi.
15
Sio masihara jadi,
Ni kitu hakina budi,
Kutunzwa kwa jitihadi,
Moyo wangu wamaizi.
16
Sisi tusio na kitu,
Katika maisha yetu,
Jadi mali bora kwetu,
Kudharau ni upuzi.
17
Si tayari kwa kutupa,
Hata kama kutanipa,

Furaha na kunenepa,
Na ufalme na enzi.
18
Ningestahabu jadi,
Kuliko kupata sudi,
Ya dhahabu na nakidi,
Kukidhia matumizi.
19
Niliitupa kijana,
Wakati akili sina,
Sasa sikubali tena
Nijapopewa feruzi.
20
Kabla ya kutumika,
Maandiko Afrika,
Kuimba tulisifika,
Kwa nyimbo na tumbuizi.
21
Nilipokuwa kijana,
Ingawa nilikazana,
Kama hili sikuona,
Naliona siku hizi.
22
Lingefanya majilio,
Wakati nguvu ninayo,
Ningeacha nyuma nyayo,
Ambazo hazipotezi.
23
Ningemwachia alama
Waone wajao nyuma
Asaa iiwa njema

Kwao kama maongozi
24
Yana ajabu maisha
Yakikaribia kwisha
Ndipo yanapoamsha
Fani mashazi mashazi
25
Na jua letu likichwa
Na mvi katika kichwa
Mioyoni twachokochwa
Haja zetu hazituzi.
26
Wakati wakwenda mbio,
Maisha kwenye kituo,
Twapata wakati huo,
Maono jozi kwa jozi.
27
Na ijapo mansubu,
Akili ya kuratibu,
Mambo kwa utaratibu,
Mwili hauwezi kazi!
28
Tunapojiwa na lubu
Na akili mujarabu,
Mwili twaona tabu
Kutumia hatuwezi.
29
Na tukiwa tabuni
Hatuna nguvu mwilini,
Ndipo ijapo kichwani,
Akili iliyo razi.

30
Maisha yetu mafupi
Na sijui twenda wapi
Mambo yatakua vipi,
Kama hima sifanyizi.
31
Tunaishi na kuhama,
Lazima nifanye hima,
Maana kifo daima
Hutokea kama mwizi.
32
Dibaji ikome hapa,
Kwa sababu nina pupa,
Na haraka yakuwapa
Habari bila ajizi.
33
Kama nitaajizika
Na mambo yatajizika,
Yawe dhiki kuchimbuka,
Yasumbue wachimbuzi.
34
Ni heri nifululize
Nisikwae niteleze
Kila baya nilimeze,
Jema niwapewapenzi
35
Kisa cha huu utenzi
Ni kuyahami mapenzi,
Hata nikiwa mpuzi,
Nia hii sigeuzi.
36

Nia yangu sigeuzi,
Sitishwi na pingamizi,
Nitanena wazi wazi,
Niachie waamuzi.
37
Wimbo wangu taachia ,
Watu wema uamua,
Sina haja kuamua,
Kupitisha maamuzi.
38
Taachia wenginewe,
Penye kosa wakosoe
Lakini mimi mwenyewe
Kufanya hivyo fauzi.
39
Ni upuzi kukashifu,
Natenda kwa taklifu,
Walakini kusharifu,
Mambo nina mazoezi.
40
Mapenzi nitayasifu,
Mpaka sikku ya ufu,
Maana ndio turufu,
Kwangu ilivyo azizi.
41
Sita zake nitapanga,
Kwa fikira za kuwanga,
Na manene venve anga,
Yatajaa beti hizi.
42
Beti nitazishibisha

Maneno va mshavasha
Mema kwa kuchangamsha
Kama siki kwa mchuzi.
43
Maneno niliyo nayo,
Nitafuma yawe nguo,
Niupambe wimbo huo,
Kama mwili wa mavazi.
44
Nitaupamba kwa pambo,
Wimbo upendeze umbo,
Walie wivu warembo,
Wa misri na Hijazi.
45
Wivu walie ulaya,
Watu waelewa sana,
Kila pembe ya dunia,
Jumla waturiga lenzi.
46
Mapenzi kwangu uhai,
Kila mara hukinai,
Kama ninywae divai,
Baridi katika kuzi.
47
Kama ninywae asali,
Tamu sana ya asili,
Au kitu cha halali,
Kipendezacho mwenyezi.
48
Atafutae malau,
Si mwerevu ni bahau,

Kuyavunja kwa nahau,
Mapenzi mtu hawezi.

49
Anambiaye hapendi,
Njia moja naye sendi,
Nashuku kanywa mtindi,
Mawazo mema hawazi.

50
Nahofu kanywa kangara,
Kileo chenye madhara,
Na fikira zimegura,
Kuzingatia hawezi.

51
Nawaza kanywa uchungu,
Moyo wake unasugu,
Ama umemea gugu,
Haoni wala hawazi.

52
Nakisi kalewa mbege,
Na sawa mtu bwege,
Mapenzi tunda za ndege
Wanyama na sisimizi.

53
Naona kalewa moshi,
Akili hazimtoshi,
Na mimi hanishawishi,
Kuwa wake mwandamizi.

54
Huenda kavuta bangi,
Fahamu yake si nyingi,
Hawazi wala hawangi,

Hajui la matumizi.

55

Hakosi kanywa zarambo,
Yawaka katika tumbo,
Kisha haelewi mambo,
Kama mwenye jinamizi.

56

Huwa kalewa kasumba,
Fahamu yake utemba,
Hudhani kuwa huimba,
Kumbe hulia machozi.

57

Nadhani kalewa mvinyo,
Yuko ng'ambo ya maonyo,
Mjeledi na msonyo,
Kumfunza haviwezi.

58

Nahisi kuwa konyaki,
Kwake ni kama rafiki,
Nayo humpinga haki
Bali bado kumaizi.

59

Labda hana la kweli,
Majuruhi wa akili,
La dhambi na la adili,
Kupambanua hawezi.

60

Pengine hana fahamu,
Si mtu mwenye elimu,
Kad ya mambo muhimu
Mapenzi hayana mwenzi.

61
Kati ya mambo mazuri,
Mapenzi kwangu fahari,
kUshinda hata Johari,
milki ya wenye enzi.
62
Mapenzi kwangu kileo,
Cha thamani hata cheo,
Nikinywa hutuza moyo,
Josho langu la kutuzi.
63
Si wa wazo wala njozi,
Si wa feli za ujuzi,
Wala si mtu wa maize,
Mdhalilisha mapenzi.
64
Si wa rai na fikira,
Wala tembe wala tijara,
Si wa hukumu imara,
Mjinga wa utambuzi.
65
Si wa neno la hekima,
Wala wazo la kupima,
Hawazi jambo la wema,
Si mtu wa fafanuzi.
66
Ulimwengu kama huu,
Wenye mashaka makuu,
Kimbilio la nafuu,
Ni palipo na mapenzi.
67

Si kwamba nabahatisha,
Kweli tupu napitisha,
Hayana kitu maisha,
Kama hayana mapenzi.
68
Tungekosa kuwa nayo,
Mapenzi kadka moyo,
Dunia tuliyo nayo,
Ingesumbua wakazi.
69
Ingemshimda wakaaji,
Kwa kukosa kufariji,
Mapenzi wanahitaji,
Watu kama ukombozi.
70
Laity si kitu hiki
Pangekuwa pana dhiki,
Dunia haikaliki,
Kwa uzito wa majonzi.
71
Dunia tunayokaa,
Jangwa tupu la ukiwa,
Na kiu na njaa mbaya,
Na mateso na machozi.
72
Kama si Johari hii,
Mashaka yake uhai,
Kuchukua natumai,
Tungekua hatuwezi.
73
Na tena yangesumbua,

Watu yakawalemea,
Maisha waliyopewa,
Yangekua kama njozi.

74
Yangalikua si kitu,
Kwa mnyama wala mtu,
Katika huu msitu,
Wa giza na pingamizi.

75
Kwa hivi ninatukuza,
Kadiri ninavyoweza,
Mapenzi yameeneza,
Ulimwenguni ulinzi.

76
Hadithi za usifiwa,
Nyingi katika dunia,
Kama zikiangaliwa,
Ndaniye yamo mapenzi.

77
Hazina mahali pisi ma,
Pa kuanza na kukoma,
Lakini zimo daima,
Ndani yake hili zizi.

78
Ndio msingi wa jingo,
La hadithi na utungo,
Na tena ndio mlango,
Mkubwa wa uokozi.

79
Kama haziishi humu,
Huwa si hadithi tamu,

Na mambo yake magumu,
Tisho na maangamizi.

80
Hili nimepeleleza,
Kugundua nikaweza,
Na leo nalieleza,
Kwa maono yangu wazi.

81
Mapenzi ni uokovu,
Utiao roho nguvu,
Zikkaenda kwa utuvu,
Safari ya utelezi.

82
Na safari ya maisha,
Kwa hali inavyotisha,
Kwenda ingalituchosha,
Mungu bariki mapenzi.

83
Tusingalikwenda mwendo,
Wala kulitenda tendo,
Zingekua ni mawindo
Roho zetu ya chukizi.

84
Mbingu ilivyo na taa,
kama ya mwezi na jua,
Na mwanadamu kapewa,
Nuru hii ya mapenzi.

85
Mawalii na watawa,
Jangwa hili la uiwa,
Daima hujiandaa,

Wapate hava majazi.
87
Mapenzi kwa,
Mwanadamu,
Kama mshipa na damu,
Na mfupa kwa shahamu,
Au mti na mzizi.
88
Dunia jangwa la kiu,
Na sisi tusisahau,
Mapenzi faraja kuu,
Yakuzima kiu hizi.
89
Tutafute tuyaone,
Tugawane tonetone,
Na yatutibu tupone,
Maradhi yenye chukizi.
90
Wahiniyo kupendana,
Dunia ingawa pana,
Huwa watu wauona,
Nyembamba na kama uzi.
91
Huwa hawana nafasi,
Kwa chuki na wasiwasi,
Hupata wakajihisi,
Kuwa ni watu wapuzi.
92
Dunia ilivyo ngumu,
Mtu hataweza dumu,
Wakati wakulazimu,

Kutoweka kwa mapenzi.
93
Siku hiyo tutajuta,
Kwa msiba kutupata,
Nyuso zetu zitatota,
Kwa bahari ya machozi.
94
Nyuso zitafanya mito,
Yamachozi ya fuuto,
Tulie kama watoto,
Masikini wa walezi.
95
Masikini na tajiri,
Watu wakila umri,
Kulia watakithiri,
Kama hili hubarizi.
96
Watalia:ole mama!
Wajile wenyewe nyama,
Wakati wa kutazama,
Hapana tena mapenzi.
97
Kwa mioyo kukauka,
Hakuna tena kucheka,
Kwa furaha kutowekka,
Wote katika majonzi.
98
Mapenzi yakishahama,
Na huruma kuandama,
Watageuka mabuma,
Watu wa zamani hizi.

99
Kwa meno kujitafuna,
Na kila uso kununa,
Fedheha hapana tena
Kwa utovu wa mapenzi.
100
Mapenzi watatafuta,
Kila njia watapita,
na nyayo zimejifuta,
wapotewe na pumzi.
101
Pumzi zikishapaa,
Pataua na fazaha,
Na ngasiya na butaa,
Dhiki na maangamizi.
102
Baada ya kuhasiri,
Hapatakua na siri,
Kulia watakariri,
Wazaliwa na wazazi.
103
Wote wapige mayowe,
Mapenzi wayalilie,
Kwa kutaka yarejee,
Na kurudi hayawezi.
104
Watayataka kwa pesa,
Yawape tena fursa,
Kitu walichokifyosa,
Hawaje tena kipenzi!
105

Watayaita mapenzi
Waitikwe na chukizi,
Wawe katika majonzi,
Ya giza nay a kilizi.
106
Ni desturi ya watu,
Walicho nacho ni siu,
Tena kawaida kwetu,
Kutaka cha kutuhizi.
107
Hutaka cha kuwadhuru,
Kila mara na kufuru,
Lakini cha kunusuru,
Hata tembe hawawazi.
108
Hubuniwa zanamzo,
Za madhara na mizozo,
Na watu huzwa tuzo,
Ulaya nan chi hizi.
109
Hutuzwa kwa vyeo bora,
Migogoro na madhara,
Ziwapi zetu fikira
Kama watu watambuzi?
110
Tukishapata hasara ,
Huwa watu wa busara ,
Maisha ni masihara,
Kama una utambuzi.
111
Basi wakati ujapo,

Bila shaka papo hapo,
Ningetaka kuwa sipo,
Kuvumilia siwezi.
112
Ni heri nitangulie,
Kwanza kuondoka mie,
Ndipo hilo litokee,
Liwe si utangulizi.
113
Lugha hii haigombi
Kuwa mapenzi ni dhambi,
Ndipo hafanya usumbi,
Wakutunga beti hizi.
114
Kwa bahari za mapenzi,
Nasema maneno wazi,
Si ubembe na upuzi,
Shauku na ubabzazi.
115
Mi nasema kiini,
Malkia wa moyoni,
Na Johari ya peponi,
Wakati wa maamuzi.
116
Mapenzi niyanenayo,
Ya saburi na makao,
Milele katika moyo,
Si mapenzi makimbizi.
117
Mapenzi yenye udumu,
Milele yaliyo tamu,

Moyonimwa mwanadamu,
Husema kurasa hizi.
118
Ni yale yautakaso,
Ngao yetu yamateso,
Yakabiliyo kwa uso,
Mbalimbali mageuzi.
119
Mapenzi yenye uzuri ,
Na thamani na fahari,
Mapenzi Al-khadhir,
Si mapenzi bumbuwazi.
120
Sio yapigayo mbio
Wakati wa majilio,
Ya msiba na kilio,
Ukabaki bila mwezi.
121
Ni mapenzi ya mitume,
Yaliyoshinda kinyume,
Nasisi tufanye shime,
Kuandama nyayo hizi.
122
Tusihini walimwengu,
Mapenzi tumpe mungu,
Naye atatupa fungu,
Katika wake wenezi.
123
Tupendane na wenyewe,
Tofauti tuondoe,
Amani itushukie,

Mapenzi tufanye ngazi.
124
Yawe ngazi ya kupanda,
Juu wakati wa kwenda,
Roho zetu kwa kushinda,
Dhiki ya mwili na ngozi.
125
Silika ya upendana
Ni mila kwa waungwana,
Kisha jambo bora sana,
Kazi bure ubaguzi.
126
Ubaguzi ni husuda,
Wala hauna faida,
Unadhuru kila muda
Katika kila kizazi.
127
Kuchukiana ni ila,
Madhara ya makabila,
Yaliyofanya ni mila ,
Yameona mapinduzi.
128
Hata lini mataifa,
Maarufu yenye sifa,
Yatatangua kashifa,
Hii sawa na masizi?
129
Mapenzi ya idhilali,
Kuwa nayo afadhali,
Bali mtu hahimili,
Wepesi wenye chukizi.

130
Chuki nnaiona nzito
Kuchukua ina moto,
Kuhesabu kama pato,
Moyo wangu umeizi.
131
Mapenzi hububu moja,
Kuwa nayo ninahaja,
Maana ndiyo faraja ,
Bora kwangu haiozi.
132
Chuki ina uharabu,
Mama wa kila aibu,
Hata hapewa dhahabu,
Kuchukua ningeizi.
133
Ningekaa na kitu hiki,
Moyo wangu hautaki,
Heri uishi na dhiki,
Utumwani wa mapenzi.
134
Ni heri uwa mfungwa,
Gerezani nikanyongwa,
Kuliko kuwa mtengwa,
Mbali yah ii feruzi.
135
Chuki sipendi kuona,
Kitu hiki cha laana,
Ni sumu ya kuungana,
Kwa roho zake mwenyezi.
136

Chuki uchafu wa moyo,
Ni hasara kuwa nayo,
Walio na mahusio,
Huikana kuwa mwenzi.
137
Penye mapenzi mapana,
Hasama huwa hapana,
Natuhuma na fitina ,
Kuja hapa haviwezi,
138
Hubwaga moyo na joyo,
Mapenzi aliyenayo,
Nijambo bora upeo,
Kinyume hakitokezi.
139
Ni himaya penye thiki,
Kwa ndugu na marafiki,
Hasa mapenzi ya maki,
Ambayo si makimbizi.
140
Ni Johari ya thamani,
Kwa kuunga majirani,
Kama watoto nyumbani,
Wanasaba wa uzazi.
141
Ni jambo halina ila,
Kwa wanaopenda mila,
Na wenye kumcha mola,
Maliki na wenye enzi.
142
Mapenzi kila yalipo

Na Amani huwa hapo,
Lakini ila ilipo,
Chuki pana uchokozi.
143
Kuna giza na msitu,
Baa na fujo na kutu,
Moyo usopenda mtu,
Si moyo uliowazi.
144
Huwako kwa,
Mwanadamu
Uharibifu na sumu,
Dhuluma na uhasimu.
Kama kupenda hauwezi,
145
Huwa mwingi wa maovu,
Moyo wake mpotovu,
Na hiyana na utovu,
Wa Imani na mapenzi.
146
Mwenye chuki masikini,
Ni mtu hana thamani,
Malaika wa mbinguni,
Chuki hawaitukuzi.
147
Mapenzi wanayo mengi,
Wanadamu kila rangi,
Lakini hayawaungi,
Kwa sera ya ubaguzi.
148
Wa ulaya wamba bora,

Asiya wamba tohara,
Marekani masogora,
Haja yao si mapenzi.
149
Hindi na bara arabu,
Wamba wastaarabu,
Yahudi jadi vitabu,
Mapenzi kwao upuuzi.
150
Na wang'ambo ya dunia,
China na Australia,
Huwa kwao maridhawa,
Maisha bila mapenzi.
151
Tanganyika na ajjemi,
Watu kimya hawasemi,
Lipi bora kwa kuhami,
Mapenzi au chukizi.
152
Mapenzi mim nahisi
Hupendeza kwa warusi,
Na ambao kwamba asi,
Tamthiliya ya wokozi.
153
Chuki jambo la udhia,
Si jema kutaradhiwa,
Na kama litaridhiwa,
Tutamezwa na ushenzi.
154
Si vyema kurudi tena,
Ushenzi wema hauna,

Lakini dawa hapana,
Ila sera ya mapenzi.
155
Nenda nchi za mapenzi,
Na vinywaji vya ujuzi,
Zinazara nchi hizi,
Nenda bila ya ajizi.
156
Nazimiliki dhahabu,
Nchi za chuki aibu,
Kuziishi si thawabu,
Hazifaikwa makazi.
157
Maziwa na majohari,
Na miski na ambary,
Utajiri na fahari,
Yote sawa na upuuzi.
158
Kuwe na mito ya lulu,
Na yakuti zisihulu,
Watu shida kufaulu,
Yakiwa duni mapenzi.
159
Ziwe na wingi wa mali ,
Uzuri ila pahali,
Huwa hazina fadhili,
Nchi hizo kwa wakazi.
160
Nchi ziwe na idadi ,
Ya vito na zumaridi,
Zisiporidhi fuwadi,

Kwa watu hazipendezi.
161
Hupendeza kuwa nayo,
Mapenzi ua la moyo,
Ambayo hauna choyo,
Wala feli za ushenzi.
162
Kwa kuja haribu kitu,
Ugomvi hauthubutu,
Wala matata ya mtu,
Kwa walio na mapenzi.
163
Mashaka yetu ya leo,
Na ya wakati ujao,
Hatuna zuio nayo,
Kama hatuna mapenzi.
164
Mapenzi yaliyo safi,
Kama hatuna ukufi,
Ghasia na ukorofi,
Kuepa hatuviwezi.
165
Milele huundwa zana,
Kwa watu kuogopana,
Kazi yoyote hazina,
Ila ya maangamizi.
Si dawa kuwa na zana,
166
Kama mapenzi hapana,
Kwa sababu hatapona,
Ateswaye na chukizi.

167
Kila mpakata moto,
Mfano kama mtoto,
Hadai kupata pato,
Zaidi ya maunguzi.
168
Kama wasio na macho,
Hawaoni watendacho,
Wala wakifikiricho,
Kwa kuunda zana hizi.
169
Nusura ya kuwa bubu,
Kwa ukubwa wa ajabu,
Uasi na uharabu,
Kuwa na maandamizi!
170
Sawa na wenye wazimu,
Na akili si timamu,
Ndipo wakawa na hamu,
Ya ghasia kama hizi?
171
Jibu la hili sipati ,
Wala wacu siwakuti,
Wenye rai madhubuti,
Yakunituza pumzi.
172
Kwenda mbele wamezidi,
Kwa elimu na juhudi,
Kwa adili wanarudi,
Tena katika ushenzi.
173

Hifadhi haina budi,
Na kupigwa wakaidi,
Lakini kila fuadi,
Rutuba yake mapenzi.
174
Watu kuwa na kivuli,
Bila Amani si kweli,
Lakini juu hili,
Manenzi kitu azizi.
175
Watu wakiwa wapendwa,
Na kila haki kulindwa,
Kabla ahera kwenda,
Pepo hapa watahozi,
176
Na roho ziwapo radhi,
Hapa katika ardhi,
La shari na la mauhi,
Litapingwa kubarizi.
177
Wa watu wenye mahaba,
Neema haziwi haba,
Kia hheri ya ushiba,
Wanayo atia zizi.
178
Bure kuwa na akili,
Elimu ya kila feli,
Huzidi kuwa jahili,
Maskini wa mapenzi.
179
Mapenzi huunga mbingu,

Ardhi na walimwengu,
Mbele ya hasimu wangu,
Huweza kunipa enzi.
180
Kwa hivi na tujiase,
Kupendana tusikose,
Na mioyo tutakase,
Kwa uturi wa mapenzi.
181
na tufue kama nguo,
kuwa safi kila moyo,
na tungoje majilio,
ya mapenzi na kutuenzi.
182
Majilio nayaona,
Yanauja mbio sana,
Na karibu tutapona,
Kama ni watu maizi.
183
Tufue kama libasi,
Roho zetu na nafsi,
Ziwe makao halisi,
Ya furaha na ujuzi.
184
Moyo uwe bustani,
Mapenzi yameendani,
Tuwe na matumaini,
Baraka zile na hizi.
185
Baraka tusizingoje,
Haraka twataka zije,

Dunia mwaionaje,
Ilivyo na kalamzi.
186
Nuru yetu ya mapenzi,
Haina anga la mwezi,
Bali ina maongozi,
Ajabu yake mwenyezi.
187
Haina anga la jua,
La kuchwa na la kupaa,
Liamshalo dunia,
Na kulaza usingizi.
189
Haina anga la nyota,
Zuri za kumeremeta,
Lakini likimvuta,
Mtu moyo hageuzi.
190
Nuruye si ya fahari,
Mfano kama sayari,
Bali mola mashuhuri,
Huyatukuza mapenzi.
191
Mwenye wakia mapenzi,
Sawa na mwenye kuhozi,
Kitu kilichon azizi,
Na halali na kipenzi.
192
Mapenzi ya tone moja,
Moyoni huwa faraja,
Kuliko vyeo korija,

Na nishani jozi jozi.
193
Na ujinga wa kupenda,
Si werevu wa kutenda,
Kila hila ya kushinda,
Wanadamu kwa chukizi.
194
Chuki ni kama nyamafu,
Ina vundo la harufu,
Na madhara maradufu,
Kwa watu haipendezi.
195
Kitu chenye maudhiko,
Na fujo na masumbuko,
Dhiki na masikitiko,
Kuwapo dingamiz.
196
Jambo tusilolitaka,
Huhimizwa kuondoka,
Kwa mni tunalotaka,
Kuja hatulihimizi?
197
Chuki kuwa kati yetu,
Sioni twatenda kitu ,
Wenyewe wanyama,
Mwitu,
Sisi hsitupendezi.
198
Twacheka na malaika,
Huchekwa na tukachekeka,
Mashetani na mizuka,

Hutuona ni wapuzi.
199
Twacheka kwa kuhizika,
Hatuna la kutamka,
Huchekwa tukianguka,
Kunyanyuka hatuwezi.
200
Twachekwa kwa ulegeu,
Akili yetu si pevu,
Twachekwa kwa upumbavu,
Wa thamani ya mapenzi.
201
Tunachekwa na wadudu,
Wajinga kwa kuabudu,
Na ambao hawamudu,
Kwamba wala kumaizi.
202
Chuki inatugawanya,
Amani hutunyang'anya,
Na haki hutupokonya,
Yetu katika mapenzi.
203
Miyo yetu na utu,
Wanayo wanyama mwitu,
Na yao sasa ni yetu,
Ni upeo wa majonzi.
204
Haya kwetu zimehama,
Zimekwenda kwa,
Wanyama
Fundi wa maneno mema,

Matendo hayatuwezi.
205
Chako jilie mwenyewe,
Huna haja ukigawe,
Bali mapenzi nipewe,
Chochote hayapunguzi.
206
Kupunguza shida sana,
Kupendana ni ungwana,
Na ye yote hatakana,
Mwenye maarifa razi.
207
Hazina yakke mapenzi,
Haishi kwa matumizi,
Mwenye masrifs razi,
Kupinga hili haliwezi.
208
Hasha usinipe kitu,
Kinachohwa na kutu,
Kwakowe nataka utu,
Utu wema hauozi.
209
Bilashi unipa fedha,
Bure itanipa adha,
Nipe kitu mfawidha,
Ambacho hushinda wezi.
210
Na kisha sinipe mali,
Usumbufu wa akili,
Nipe mapenzi halali,
Yasumbue wachopozi.

211
Wala sihitaji sifa ,
Riziki ya wenye kufa ,
Nipe dawa ya maafa,
Wakati nina pumzi.
212
Mimi sifa za dunia,
Sina haja kusikia,
Sababu zinahadaa,
Na wingi wa mapinduzi.
213
Ingawa ni kitu chema ,
Sikio langu huuma,
Iwapo sifa yavuma,
Kuwa imara siwezi.
214
Siwezi kwa kuchukua,
Mara nyingi hulemea,
Na begani huchubua,
Mimi siwi mchukuzi.
215
Kisha hudhuru mabega,
Sifa haina kiaga,
Wangapi imewabwaga ,
Wenye kutaka ihozi?
216
Sifa kitu cha duara,
Haishiki imara,
Wenyewe watu sogora,
Kwa maarifa hyerezi.
217

Sifa kitu cha shukuki,
Kama tupu hailiki,
Sifa huudhi rafiki,
Ukawindwa kwa kitanzi.

218

La sifa halinandani,
Na mbele silitazami,
Asiyependa ni mimi,
Wengine siwakatazi.

219

Wapendao na wapate,
Ziwapambe mwili wote,
Mimi zisinifuate,
Sina haja kuzihozi.

220

Si kitu cha kutamani,
Sifa ina ushindani,
Na wivu na nuksani,
Na aibu na machozi.

221

Ujapo pata wa juu,
Heri kwako kusahau,
Sifa kiburi kikuu,
Kwa ambaye haiwezi.

222

Ni jambo halinifai,
Sifa ina ulaghai,
Ni silaha ya uadui,
Aili na majambazi.

223

Sifa apendaye hasa

Hutekwa moyo kabisa,
Akatenda kila kisa,
Ghairi ya kizuizi,
224
Kwa ghiliba ya nafsi,
Huwa hanacho kiasi,
Hasikilizi la kusi,
Halichi la kaskazi.
225
Halichi la mashariki,
Wala neon la rafii,
Kwa sifa kumpa dhiki,
Hawazi wala hatunzi.
226
Na ya watu hayamwimbi,
Hajali la magharibi,,
Hutenda kila hitimbi,
Bila ya kuwa mjuzi.
227
Katika kutenda feli,
Sifa haina zohali,
Hutenda bila kujali,
Gharika wala utelezi.
228
Sifa kitunga cha jicho,
Huoni ukiwa nacho,
Udhanicho huwa sicho,
Hupati jambo la wazi.
229
Na mara kwa mara sifa,
Haisikii la kufa,

Wala lenye maarifa,
Chacheya uangalizi.

230
La rahisi huwa ghali,
Kama sifa yakubali,
Kama yabadili hali,
Sifa kupinga huwezi.

231
Kwa hiyo najitanibu,
Sikai nayo karibu,
Isije kunighilibu,
Mambo yake siyawezi.

232
Nipe mapenzi niweke,
Moyoni pahali pake,
Nilinde yasifujike,
Kwa doria ya ulinzi.

233
Niyalinde kwa doria,
Mwivu asipate njia,
Ndogo yakuyachukua,
Kwa rai na upekuzi.

234
Nipe niweke kwa siri,
Mapenzi hutaka ari,
Na moyo wa ujasiri,
Kukabili shambulizi.

235
Bila kudokoa mvivu,
Yakue yawe nguvu,
Mpaka yawe mapevu,

Yazidi kuwa azizi.
236
Na yapambe kila moyo,
Kila mtu awe nayo,
Pasiwe mlia choyo,
Watu wote wayahozi.
237
Mapenzi yawe na umbo,
Yapendeze kwa warembo,
Na waelewa wa mambo,
Mahiri na watatuzi.
238
Yaenee kila nyumba,
Kwa wanene na
Wembamba,
Watu wote kuwapamba,
Tamthilia ya raavazi.
239
Yawe mengi duniani,
Tujue yake thamani,
Sote tuwe furahani,
Pasiwe mlia chozi.
240
Mapenzi yawe mwangaza,
Kwa wajuzi wa kuwaza ,
Wajue la kutukuza,
Na lililo la upuuzi.
241
Yawe ndani ya fuadi,
Za watu wote weledi,
Na kila siku Yazidi,

Kumea kama mizizi.
242
Yawambe kama mimea,
Kwa majani na maua,
Na matunda yakuliwa,
Mfano tende na lozi.
243
Mapenzi pambo moyoni,
Kwa wafupi wastani,
Na warefu makundini,
Raisi na wanagenzi.
244
Wanagenzi na raisi,
Katika zao nafsi,
Watu wa kila jinsi,
Mapenzi kwao feruzi.
245
Katika kutenda tendo ,
Watu wakiwa na pendo,
Hapatakuwa na kondo,
Chuki wala ubaguzi.
246
Mapenzi kitu hazina,
Kwa weledi wa maana,
Watu wakila namna,
Wari na wakurugenzi.
247
Wakurugenzi na wari,
Watu wa kila kadiri,
Mapenzi kwao fahari,
Mfano mbingu na mwezi.

248
Pendo likiwa pahali,
Hufanana na kandili,
Na nuru kwa rniali,
Hapaji na virigizi.
249
Na palipo na rabsha,
Pendo ni faraja tosha,
Na rnmwili huimarisha,
Usiwe na nyong'onyezi,
250
Watu huwa na imara,
Wakawa na masihara,
Kucheka bila ghera,
Kusema bila kohozi.
251
Wenye kiu hutulizwa,
Na wagonjwa huuguzwa,
Mapenzi ni miujiza,
Mikubwa iliyo wazi.
252
Na wenye njaa hulishwa,
Yarima hufurahishwa,
Mzunguko wa maisha,
Pete yake ni mapenzi.
253
Mapenzi kwangu ni hadhi,
Si kitu cha kuniudhi,
Nanyi niwiweni radhi,
Msomapo beti hizi.
254

Sababu ya kusanifu,
Beti hizi ni kusifu,
Johari yangu tukufu,
Iwekayo moyo wazi.
255
Kwangu ina ushawishi,
Johari hii aushi,
Na moyoni hainishi,
Wala haijipunguzi.
256
Ni kito moyoni kimo,
Nacho kitadumu humo,
Kwangu haina ukomo,
Ladha hii ya mapenzi.
257
Pindi rungekuwa bia,
Kwa shirika kutumia,
Mapenzi yangalikuwa ,
Faraja kwa warumizi.
258
Sote twaweza shiriki,
Faraja ya kitu hiki,
Nacho hakifilisiki,
Ni hazina ya majazi.
259
Pande zote za dunia,
Ni hazina maridhawa,
Na kila unachotwaa,
Humo kitu hupunguzi.
260
Punji ya pendo moyoni,

Kama jua duniani,
Na huzidisha thamani,
Yake mtu kwa mwenyezi.
261
Na kwa wingi huhesabu,
Mahaba kama dhahabu,
Kitu hii mahabubu,
Kwa ambao hukienzi.
262
Kwa ambao ni maizi,
Mahiri na watatuzi,
Pulinganisha na mapenzi,
Ya watu kama pumzi.
263
Yamekutwa na mola,
Wakia ni frasila,
Na ratili ni jazila,
Kuwa ghali hayatuzi.
264
Hayana mwisho wa kima,
Na uzuri na heshima,
Kwa kila mwenye heshima,
Hana kisio la wazi.
265
Yakipimwa kwa urefu,
Huzidi kwa utukufu,
Na kwa nguvu maarufu,
Kwa watuu hayapozi.
266
Kila yakifa humea,
Na ugonwani hupoa,

Kwa hivi huendelea,
Mwendo wake hauvizi.
267
Ni kitu chenye umri,
Hawishi wake uzuri,
Na ubora na fahari,
Na wala hakichukizi.
268
Hukonda na kunenepa,
Madeni yake hulipa,
Na watu wake huwapa,
Ya fadhili na majazi.
269
Bila maji na chakula,
Huamka na hulala,
Hmshi bila ila,
Na raha hayapotezi.
270
Na mara nyingi hukidhi,
Linaridhia radhi,
Bila hutupa hadhi,
Heshima yake hadhi.
Heshima yake na enzi.
271
Kama mapenzi ya kweli,
Hayana haja ya mali,
Na wala hayaendi mbali,
Siku ya kuja majonzi.
272
Penye dhiki na msiba,
Marafiki huwa haba,

Ni ushahidi haiba,
Wa kuwa tunu mapenzi.
273
Siku ya dhiki na hatari,
Huna wa kukushauri,
Ni ushahidi Dhahiri,
Wa pendo kwa wamuuzi.
274
Hawajali ya kuona,
Kama mahaba hawana,
Wala kuwa na maana,
Maisha bila mapenzi.
275
Siku ya kuja kuhama,
Mapenzi na taadhima,
Hapatakuwa na wema,
Ila pitu na pituzi.
276
Hapatakua na tembe,
Wema katika viumbe,
Na watu wa kila pembe,
Watazama kwa machozi.
278
Chozi litatiririka,
Mfano kama gharika,
Pasiwe mweza kucheka,
Wala mtu mdakuzi.
279
Wenye kuwinda,
Huwindwa,
Na washindao hushindwa,

Wenye kupenda
Hupendwa,
Ni mwendo wa mazoezi.
280
Kwa mazoezi na mwendo,
Maandamo ya mkondo,
Chuki mwanawe ni kondo,
Sio kingine kizazi.
281
Mwaka wa kuadimika,
Mapenzi kwa kuondoka,
Moyo wangu una shaka,
Mbingu yetu kuwa wazi.
282
Hapatakuwa na kweli,
Mmoja wala wawili,
Na sheria na halali,
Kuwa lami na masizi.
283
Kama majangwa yabisi,
Ama shaba na suwesi,
Zitateseka nafsi,
Ziwe hazina pumzi.
284
Jingine ni lipi kaka,
Mapenzi yakiondoka?,
Patabaki kusumbuka,
Na msiba na simanzi.
285
Kingine ni kipi dada,
Huruma na misaada,

Sharia na kawaida,
Kama hapana mapenzi?
286
Mapenzi jambo azizi,
Werevu huweka kanzi,
Yakiiza ni simanzi,
Na kukosa hawawezi.
287
Penzi kitu cha haiba,
Aliye nacho hushiba,
Maisha bila mahaba,
Kwenda nayo hatuwezi.
288
Mapenzi kitu cha hiba,
Hasa kama si ya kwiba,
Kwetu faraja na tiba,
Ya dhiki na mageuzi.
289
Mnyonge na mshuhuri,
Maskini na tajiri,
Mlegevu na hodari,
Na mawindo ya mapenzi,
290
Na hawa wenye kuwindwa,
Huona kama walindwa,
Na kila wanalotendwa,
Kwao haliwi majonzi.
291
Mioyo huzima kasi,
Uchungu na wasi wasi,
Na ujinga wa kisasi,

Na fahari upuuzi.
292
Fahari yenye kudhuru,
Na ngumu kuamuru,
Mtu kumpa uhuru,
Na nafasi ya pumzi.
293
Mioyo huzima moto,
Pasiwe mwenye majuto,
Na watu huwa watoto,
Kwa furaha na uchezi.
294
Kwa furaha na Amani,
Watu wana tumaini,
Kwa sababu mioyoni,
Wanacho kitu azizi.
295
Bi ghairi ya mfano.
Maisha mazito mno,
Twenda nayo kwa miguno,
Mapenzi tupe pongezi.
296
Mashaka mengi tunayo,
Mazito katika moyo,
Mchana kutwa wanao,
Tuna tata na tatizi.
297
Tuna tata na tatizi,
Usiku wa jinamiz,
Si watu wa usingizi,
Wala si wa maongezi.

298
Si wenye haiba kitu,
Katika nafsi zetu,
Tumekua sio watu,
Twanuka kama kutuzi.
299
Kwa machozi hutupita,
Nyuso zetu zimetota,
Mchana kutwa twajuta,
Na usiku si.
300
Kwa mashaka na madhila,
Makubwa kila kab'la,
Si walazi wa kulala,
Katika nyakati hizi.
301
Kwa fikira kwenda mbali,
Tumerukwa na akili,
Usiku hatuna hali-
Hurukwa na usingizi.
302
Kama rumebeba vyuma,
Usingizi hupararna,
Mioyo ndani yauma,
Kwa mateso chukizi.
303
Kwa kuteswa kwa kuchizi,
Kila dawa haipozi,
Na lini tutamaizi,
Dhara ya maangamizi?
304

Pingamizi kubwa sana,
Tunazo kila namna,
Roho nafsi hazina,
Kwa uzito wa majonzi.

305
Kwa chuki kutukebehi,
Si watu wa ufurahi,
Kwa sababu hatuwahi,
Kuwa katika mapenzi

306
Kitu gani cha lawama,
Ndani ya dunia nzima,
Ambacho vvatu husema,
Ni Zaidi ya chukizi.

307
Madhara ya walimwengu,
Chuki imefua pingu,
Na kila lenye mizungu,
Na madhara na ajizi.

308
Milele huundwa zana,
Na vitimbi na fitina,
Hapana mwenye kuona,
Kwa hadaa na gurnbizi.

309
Tumewanda kwa ujinga,
Na wenyewe twajifunga,
Machoni hatuna anga,
Kwa uovu utuhozi.

310
Roho chache ya shirika,

Kwa mioyo kuchafuka,
Kwa chuki kuchafuka,
Moyoni mwetu mapenzi.

311

Mapenzi yetu ya choyo,
Yametunga magao,
Kasoro kubwa tunayo,
Nayo imo kutuhizi.

312

Katika sura ni watu,
Urembo wa umbo letu,
Moyoni wanyama mwitu,
Choyo kimetupa ganzi.

313

Hatuna cheche va anga,
Kwa kiburi na ujinga,
Mioyo kama majangwa,
Ya kiu na nyung'onyezi.

314

Choyo kimetupa ndima,
Shughuli dunia nzima,
Hapana mwenye kuhema,
Wala kuvuta pumzi.

315

Twashughulika na kazi,
Heri kuwa wapagazi,
Malipo yetu kwa mwezi,
Ni majuto na majonzi.

316

Kwa chuki kutuadhiri,
Hatuna tembe fahari,

Ya rai na tafakuri,
Kama watungulizi.
317
Sawa na watu madufu,
Wachache wa utukufu,
Na mioyo ina hofu,
Kwa ufupi wa pumzi.
318
kwa hali nama hii,
Tumekuwa hatufai,
Ingawa tuna uhai,
Mioyo yetu si wazi.
319
Hapana mwenye mwafaka,
Kwa roho kukorofika,
Afadhali ya mizuka,
Hayawani na washenzi.
320
Kwa ghiliba na uongo,
Si wazima wa maungo,
Kama wagonjwa wa jongo,
Na baridi na tambazi.
321
Kwa yabisi ya fuadi,
Si watu wenye muradi,
Kila jambo halisudi,
Hapana lenye majazi.
322
Penye mapenzi ya shida,
Sharia na kawaida,
Hutanguka bila muda,

Si pazuri kwa makazi.
323
Siku ya kuwa na mbwawa,
Mapenzi muda was aa,
Kwa watu kuyakkimbia,
Tutakufa kwa majonzi.
324
Lisijiri jambo hili,
Mungu lipeleke mbali,
Jambo hili libadili,
Haraka bila ajizi.
325
Kwa kuwa si jambo jema,
Na libadilike hima,
Kwa uwezo wa rehema,
Na busara ya mwenyezi.
326
Roho zitie rutuba,
Ya mapenzi na mahaba,
Na kweli na usuhuba,
Katika kila kizazi.
327
Kisha ziwe na neema,
Ya haki na utu wema,
Na fadhili na heshima,
Na kipawa cha ujuzi.
328
Bila hivi kukutana,
Na watu kueleana,
Kwa hali ya kupendana,
Ulimwengu ni upuuzi.

329
Kama chache ya mapenzi,
Dunia hatuiwezi,
Kama chache ya ujuzi,
Dunia maangamizi.
330
Chuki kitu hatari,
Afadhali ya ghubari,
La baridi ama hari,
Na pepo za pingamizi.
331
Kama chuki ina mwanya,
Nafasi kujikusanya,
Dhara huweza kufanya,
Ya mwaka katika mwezi.
332
Kwa muda sekunde moja,
Chuuki huweza kufuja,
Lisemwalo kwamba laja,
Hata la zamani hizi.
333
Chuki inashinda moto,
Ikisadifu mateto,
Chuki na kitu kizito,
Kuweka hatukiwezi,
334
Chuki kitu cha maudhi,
Afadhali ya maradhi,
Yana dawa na hifadhi,
Ya siri na waziwazi.
335

Chuki ghera ya moyoni,
Afadhali ya mauti,
Ni faradhi kwa umati,
Chuki ina nyong'onyezi.
336
Chuki madhara ya dhati,
Afadhali ya mauti,
Ni faradhi kwa umati,
Chuki inanyong'onyeza.
337
Hapana mtenda neno,
Wala mfanya nong'ono,
Wotw wana magombano,
Kwa madhara ya chukizi.
338
Kwa kuwamo fadhaani,
Hapana mwenye Amani,
Dogo huwa nuksani,
Kubwa huna mkombozi.
339
Twaishi dunia gani,
Hapana wa kumwamini,
Wala wa kumpa ndani,
Maskini wa mapenzi.
340
Ulimwengu wa majini,
Ama watu wenye dini,
Wenyeji wa mashetani,
Ama ya pepo wapenzi?
341
Mapenzi yetu hafifu,

Ndiye mama yake hofu,
Na baba wa upotofu,
Wazazi wa uubaguzi.
342
Fedheha kubwa kusema,
Chuki iliyo kwa uma,
Afadhali ya wanyama,
Hayawani wa ujuzi.
343
Yale kule kwa wanyama,
Mapenzi yametuhama,
Na chuki hutuandama,
Mbio hatuna pumzi.
344
Yale kule kwa wanyama,
Mapenzi yametuhama,
Na chuki hutuandama,
Mbio hatuna pumzi.
345
Chuki yenyewe laana,
Wanyama kila namna,
Mwituni wenye kulana,
Kwa watu haipendezi.
346
Chuki ni maangamizi,
Na kama tunaienzi,
Ni lazima kutuhizi,
Hili ni neon la wazi.
347
Si haja kuwa mwalimu,
Jambo hili kufahamu,

Rahisi si neon gumu,
Mpaka kwa mwanafunzi.
348
Si neon lenye gharama,
Na juhudi ya kusoma,
Liwazi kwa maamuma,
Japo kusoma hawezi.
349
Si sharti ya mahiri,
Mwelewa wa tafsiri,
Kila mwenye tafakuri,
Mara huuwa mtambuzi.
350
Kwa hakika jambo hili,
Halihitaji akili,
Kufahamu kuwa kweli,
Si gumu wa kumaizi.
351
Bila kuwa na busara,
Na fahamu kuwa bora,
Hata mwanagenzi mara,
Huweza kuwa.
352
Mapenzi hifadhi kwetu,
Furaha kwa kila mtu,
Kiungo bora kwa watu,
Hapana kama mapenzi.
353
Yana fadhili kwa watu,
katika maisha yetu,
Amani kubwa kwa mtu,

Ipi kushinda mapenzi?

354

Mapenzi kwa mtu cheo,
Huambatana na moyo,
Na mtu kama anayo,
Ana namna ya kazi.

355

Mapenzi ni hadhi wetu,
Kuwa pamoja nawatu,
Moyo hauwi na kutu,
Wenye tone la mapenzi.

356

Mapenzi ndivyo halisi,
Kuambatana na sisi,
Ni imara ya nafsi,
Kama mti kwa mzizi.

357

Mapenzi kwetu wajibu,
Yamo katika hesabu,
Ya vilivyo na thawabu,
Na majaziye mwenyezi.

358

Kwetu pendo ni fahari,
Na hazina ya Johari,
Kwa fakiri na tajiri,
Na mapenzi si machaguzi'

359

Kwa fadhili ya mahaba,
Moyo huwa na rutuba,
Kwa wingi wa masuhuba,
Na wandani wa mapenzi.

360
Kwa pendo na urafiki,
Moyo hauyabisiki,
Na kwa usawa na haki,
Huwa machache majonzi.
361
Wenye kupenda rafiki,
Nao kupendwa ni haki,
Na wenye kutaka chuki,
Hufa ndani ya chukizi.
362
Nafsi huwa nyepesi,
Kama mtu hajighasi,
Na huwa na wasi wasi,
Akiwa hana mapenzi.
363
Ikiwa watu hawamo,
Katikati ya mapimo,
Majonzi huzidi kimo,
Wakatowa na machozi.
364
Akiwa katika choyo,
Mtu fahamu anayo,
Kadiri hali iwayo,
La mapenzi haliwezi.
365
Choyo kikishika macho,
Mtu haoni alacho,
Na kila atendewayo,
Kwake hakina mapenzi.
366

Clioyo kikishika kinywa,
Mtu hali wala kunywa,
Kisha hapendi kuonywa,
Mambo yenye maangazi.
367
Choyo kikishika nia,
Mtu huwa hana njia,
Wala shauri la kuwa,
Na nyenzo na tafanuzi.
369
Choyo kikishika tumbo,
Mtu katika kiambo,
Huchafukiwa na mambo,
Ya fikira na ya kazi.
370
Choyo kikishika kichwa,
Tumia kutwa na kucha,
Kwa bidi kama mchwa,
Huna jambo la majazi.
371
Choyo kikishika uso,
Mtu hawi na takaso,
Japo mpambe kwa leso,
Batini huwa si wazi.
372
Choyo kikishika kondo,
Haba natasi ya tendo,
Na safari ya mwenendo,
Mtu kutenda hawezi.
373
Choyo kikishika rai,

Na ghera na uadui,
Hupati la kukinai,
Si mtu wa maenezi.
374
Choyo kikishika bero,
Kamili huwa kasoro,
Ukawa mtu wa kero,
Palipo na maongozi.
375
Choyo kikishika wivu,
Ni heri ya mpumbavu,
Huweza kuwa mwerevu,
Wivu giza la ujuzi.
376
Tembe huwa kubwa mno,
Choyo kikishika neno,
Huwa ghali mapatano,
Kila siku uchokozi.
377
Hutengwa na marafiki,
Choyo kikishika haki,
Huna wa kukuafiki,
Wala kuwa wako mwenzi.
378
Choyo kikishika mila,
Hakimpi mtu kula,
Wala nafasi kulala,
Hurukwa na usingizi.
379
Choyo kikishika ngoa,
Huna raha ya dunia,

Na kila linalokua,
Huwa tata na simanzi.
380
Choyo kikishika fihi,
Hupati la kufurahi,
Wala neno la sahihi,
Na la haki huumaizi.
381
Choyo kiishika hpngo,
Na maisha ya uongo,
Hupati fanya maringo,
Kwa dharau ya wabezi.
382
Choyo kikishika wazo,
Bila ya matengenezo,
Jiandae kwa mizozo,
Jambo jema hutimizi.
383
Choyo ni dhara ya kazi,
Na harabu ya mapenzi,
Choyo hakitengenezi,
Kwa wingi wa pingamizi.
384
Kama wanyama wa mwitu,
Choyo huwatenga watu,
Na pendo kiungo chetu,
Kama roho na pumzi.
385
Choyo sifaze ni hzi,
Nyingine hakitimizi,
Bora kuwa na mapenzi,

Ndicho kitu hakiozi.
386
Mapenzi yana mwangaza,
Ni taa katika giza,
Na kitu cha kutukuza,
Kila palipo wakazi.
387
Mambo mema hunijaza,
Kwa kunipa miangaza,
Na njia za kuongoza,
Zenye heri na ijazi.
388
Yana Baraka na mimi,
Nikiwa nayo sizami,
Na chuki hainifumi,
Tena siwi na kajonzi.
389
Kwangu mapenzi si adha,
Yana heri mfawidha,
Kila siu yana ladha,
Si kitu cha gagamizi.
390
Kwa mpenzi kunivuta,
Po pote ninapopita,
Moyo wangu hukutaka,
Kama maliki wa enzi.
391
Sina jambo mahasusi,
La kuniridhi nafsi,
Chochote huniandisi,
Hata kitu cha upuzi.

392
Naweza kuwa na raha,
Hata katika mzaha,
Ikawa kwangu ni jaha,
Imeshuka kwa mwenyezi.
393
Na mwili hunikunjukka,
Nikasema kwa kucheka,
Kama sinayo mashaka,
Ya njaa na mauguzi.
394
Cho chote kinachokuja,
Hata kama pesa moja,
Hutosha kuwa faraja,
Si mtu wa machaguzi.
395
Kwa wakubwa wivu sina,
Kwa wadogo kkuwaona,
Wakitaka kulingana,
Na mimi hawaniwezi.
396
Nimo ndani ya msingi,
Moyo wangu hautangi,
Walio chini ni wengi,
Kuwa na wivu siwazi.
397
Kama wengi hunipita,
Wachache hunifuata,
Na heri ninazopata,
Kwao huwa kama njozi.
398

Wa vikwi na wa idadi,
Wakipata sihusudi,
Natosheka na wahedi,
Na uzima na pumzi.

399
Kwa kutazama wa chini,
Wivu hutoka moyoni,
Na chui kuitamani,
Huwa jambo la upuuzi.

400
Kwa kutazama wa juu,
Na fahari na makuu,
Hukomi kuwa na kiu,
Na kilio na machozi.

401
Kwa kitu hata kwa hali,
Tazama watu dhalili,
Ni wangapi mbalimbali,
Wateswao na majonzi!

402
Ndani ya maisha yetu,
Wangapi wasio kitu,
Wala si wanyama mwitu,
Viumbe wake mwenyezi.

403
Wengi ni haba wa hadhi,
Na wengi wenye maradhi,
Hawana cha kuwaridhi,
Wala kitu cha kuhozi.

404
Ni wengi wenye madhila,

Hawana kitu cha kula,
Wala pema pa kulala,
Wachache wa usingizi.

405
Wengi wenye idhihali,
Hawanywi wala hawali,
Na nguo katika mwili,
Hawana Zaidi ngozi.

406
Kiwango chwa wanadamu,
Walio na shida ngumu,
Jumla ya tarakimu,
Kwa kuwanga haiwezi.

407
Hutosha kwa kila mtu,
Ulimwengu kama wetu,
Hali na tiba zetu,
Zikiwa zina mapenzi.

408
Kisha huwa hautoshi,
Kwa feli na kwa utashi,
Kama chuki huwaghashi,
Watu hawana wokozi.

409
Ulimwengu si dhaifu,
Kwa watu waadilifu,
Wa haki na ukunjufu,
Urafiki na mapenzi.

410
Na huwa kitu kichafu,
Shari na uharibifu,

Kama watu wapotofu,
Ndio wenye maongozi.
411
Ulimwengu una heba,
Amani na usahiba,
Kkwa watu wenye mahaba,
Na sikiliza za mapenzi.
412
Na huwa wenye misiba,
Na kiu ya kutoshiba,
Na aibu na ghiliba,
Kwa walio na upuuzi.
413
Ulimwengu una shwari,
Na furaha na fahari,
Kwa watu wa tafakuri,
Na wenye akili razi.
414
Na huwa wenye hatari,
Mwepesi wa kuhasiri,
Kwa asiye na nadhari,
Na ambaye hamaizi.
415
Kwa watu mwenye,
Heshima,
Ulimwengu kitu chema,
Huwa na raha daima,
Na wingi wa mapendezi.
416
Na huwa na kitu kibaya,
Kisichokuwa na haya,

Bali hasira na maya,
Dhuluma na uchokozi.
417
Kwa watu mzo kwa mzo,
Ulimwengu una tuzo,
Sifa na mabembelezo,
Mambo yake matelezi.
418
Na huwa wenye mizozo,
Na ugumu na mkazo,
Na dhiki mfululizo,
Mwendo wake hautuzi.
419
Kwa heshima na saburi,
Ulimwengu una heri,
Na Baraka na uzuri,
Na madaraka ya enzi.
420
Na huwa mwingi wa hari,
Na sakara na jeuri,
Na fadhaa na kiburi,
na mashaka na ajizi.
421
Ulimwengu kitu ghali,
Una mito ya adili,
Yenye vinywaji vya kweli,
Na ladha kushinda lozi.
422
Pengine mwingi wa feli,
Za kinyume na zohali,
N dhuluma batili,

Ghiliba na unyakuzi.
423
Ulimwengu una pambo,
Utukufu na urembo,
Na ukunjufu wa umbo,
Na anasa kwa wakazi.
424
Kisha huchafua mambo,
Kama gulio la tembo,
Ama soko ya zarambo,
Watu wakawa wapuzi.
425
Ulimwengu wa mwafaka,
Na neema na Baraka,
Na umoja na shirika,
Na uzuri wa uzazi.
426
Na pengine huchafuka,
Kama chombo kulipuka,
Pakawa mengi mashaka,
Kwa wavutao pumzi.
427
Ulimwengu wa nasaha,
Mapendeleo na jaha,
Na anasa na furaha,
Na heba ya mageuzi.
428
Kwa feli zenye karaha,
Huwa wenye majeraha,
Na tuhuma za fedheha,
Juu ya kila mkazi.

429
Ulimwengu wa uhai,
Na mambo ya utumai,
Na mashauri na rai,
Na nuru iliyowazi.
430
Na mwingi wa jitimai,
Ghadhabu na uadui,
Na fahamu kuzirai,
Watu wenye utambuzi.
431
Kwa watu wenye kutubu,
Na kuabudu wahabu,
Ulimwengu wa thawabu,
Kwa sahihi ya mapenzi.
432
Na kuahidi wa hesabu,
Za dhuluma na adhabu,
Kwa wachache wa adabu,
Na dhalimu wa wapuzi.
433
Kwa watu wenye fursa,
Ulimwengu ni anasa,
Michezo na taanisa,
Na madaraka na enzi.
434
Na huwa mwingi wa visa,
Kila dakika mkasa,
Watu wote huwafyosa,
Magunge na wanagenzi.
435

Kwa watu wenye fikira,
Na walio na busara,
Ulimwengu kitu bora,
Rahisi kwa matumizi.

436
Na hulipukwa na ghera,
Kwa ujinga na harara,
Na maudhi ya hasara,
Dhara na maangamizi.

437
Ulimwengu wa maisha,
Juhudi na mshawasha,
Na ulua na tamasha,
Na umahiri wa kazi.

438
Na huwa wenye rabsha,
Na uchovu na kuchusha,
Kwa watu wakuwazuzusha,
Kila siku mageuzi.

439
Ulimwengu wa maghaibu,
Watu wake mahabubu,
Ni ambao hujaribu,
Kuishi nayo mapenzi.

440
Hawa ni wanyenyekevu,
Bali ndiyo wenye nguvu,
Kisha huwa wapumbavu,
Lakini ndiyo wajuzi.

441
Hawa ni watu wa chini,

Lakini wana thamani,
Na ingawa masikini,
bali si watu wapuzi.

442
Wenye matendo ya wema,
Wana tuzo za rehema,
Na hadhi ya pepo nzima,
Na haki ya maamuzi.

443
Kila tendo la fadhili,
Japo likitendwa mbali,
Lina heshima kamili,
Na ushindi wa mtenzi.

444
Jambo dogo kama nini,
Na lifanyike gizani,
Lina hesabu mbinguni,
Ya mtendwa na mtenzi.

445
Na liwe jambo usiku,
Wa ng'ambo haoni huku,
La tanga ama mukuku,
Mbinguni habari wazi.

446
Ndiko kwenye madhubuti,
La kuchorwa halifutwi,
Kwa madua na kunuti,
Na maombi na machozi.

447
Kwa karatasi na wino,
Huko likichorwa neno,

Kugeuzwa gumu mno,
Hakupokewi ghawazi.
448
Kwa kufuta karatasi,
Huko hulipi fulusi,
Wala hakuna nafasi,
Ya hila wala upuuzi.
449
Na litendeke kwa siri,
Tendo na kila hadhari,
Yote kwa mola Dhahiri,
Hata dogo kama uzi.
450
Na liwe katika giza,
Bila ya kuzungumza,
Hapana cha kulimeza,
Lisende kwa wasikizi.
451
Kila kitu kitendwacho,
Hapa hakina maficho,
Yasiyofikwa na jicho,
Na hesabu ya mwenyezi.
452
Hata cha chini ya giza,
Kidogo ama kikuza,
Na kilicho na mwangaza,
Kwa muungu hakitatizi.
453
Kilicho ndani ya pori,
Ama kati ya bahari,
Kitu cha kila kadiri,

Kina hesabu ya wazi.
454
Na kitu kilicho chini,
Na mbinguni na hewani,
Hakipo yetu machoni,
Kughilibu hakiwezi.
455
Mbele yake El-kahari,
Kama hapana la siri,
Bora kutenda la heri,
Kama haki na kuyaenzi.
456
Jambo moja kwa manani,
Kama halinchikani,
Maovu faida gani,
Kupenda na kuyaenzi.
457
Ndipo hashikwa na woga,
Moyo wangu kunipiga,
Kwa kinyume na kuiga,
Yasiyoridhi mapenzi.
458
Penye mahaba na hawa,
Moyo wangu hutulia,
Pasipo na haya kuwa,
Hurukwa na usingizi.
459
Usingizi huwa ghali,
Usiku kucha silali,
Na fikira mbalimbali,
Hunijia kwa vikozi.

460
Fikira nyingine njema,
Kwa faraja na heshima,
Nyingine zina zahama,
Na husumbua pumzi.
461
Kwa mawazo kupingana,
Usingizi huwa sina,
Na fahamu ya maana,
Kupata huwa siwezi.
462
Natanga katika mbuga,
Kila kipembe kubuga,
Kitu kiwezacho roga,
Sioni kama mapenzi.
463
Pendo kama lachipuka,
Hupendwa na malaika,
Na likisha kamilika,
Humpendeza mwenyezi.
464
Pendo halirudi tupu,
Hurejea na kikapu,
Pendo lina chapuchapu,
Kuwapa watu majazi.
465
Halishindwi kila mara,
Pendo kilu cha imara,
Ndipo nikaona bora,
Kuwa wake mwandamizi.
466

Pendo ni kitu cha ada,
Na Johari ya faida,
Pendo lina misaada,
Ya daima kwa wapenzi.
467
Mapenzi pambo la moyo,
Ni furaha kuwa nayo,
Mapenzi hushinda cheo,
Hata pato la ghawazi.
468
Hayauzwi kwenye soko,
Kila pahali wendako,
Mapenzi Johari yako,
Kama nguvu na pumzi.
469
Hushindwa na kununua,
Fedha yote ya dunia,
Mapenzi robo wakia,
Haii yalivyo azizi.
470
Kwa ughali kitu hiki,
Ni sawa na urafiki,
Kupatikana ni dhiki,
Wajibu ni kukienzi.
471
Kitu hiki ni mitihaki,
Kwa waelewa wa haki,
Mapenzi dawa ya chuki,
Kwa watu wavumilizi.
472
Hayana mwisho wa ladha,

Mapenzi hushinda fedha,
Ni kitu dawa ya adha,
Ndani yana ukombozi.
473
Hushinda hata dhahabu,
Yapimwapo kwa hesabu,
Mapenzi yana ajabu,
Hayapimiki kwa wazi.
474
Hutaka wenye kwelewa,
Wajinga huwayawaya,
Pendo halifanyi kuwa,
Ladha ya mua na ndizi.
475
Yakiwa hivi mapenzi,
Hufanywa kuwa upuuzi,
Wala watu hawawazi,
476
Kuwa ni kitu azizi.
Lakini yana thamani,
Kubwa haina kifani,
Ndipo nikawa na kani,
Kuandika beti hizi.
477
Mapenzi kwangu bendera,
Na Johari ya busara,
Hunilipa kwa ijara,
Na fadhili na majazi.
478
Penye pendo nanenepa,
Mwili wangu na mifupa,

Mapenzi siwezi tupa,
Hata mwisho wa pumzi.

479
Yalipo kwangu ni raha,
Na hupona majeraha,
Ya maudhi na karaha,
Ya mwaka jana na juzi.

480
Moyoni yana thamani,
Kitu kingine sioni,
Kama hiki duniani,
Kwa mlingano wa wazi.

481
Thamani yake haishi,
Ni hazina ya uashi,
Wa watu wenye kuishi,
Maisha ya mapinduzi.

482
Mchwa wote ukutane,
Na sisimizi wanene,
Mapenzi wayatafune,
Bure watafanya kazi.

483
Na pakutane na nondo,
Na siafu hata sondo,
Hawawezi fanya tendo,
La kuyadhuru mapenzi.

484
Nzige na funza na kuntu,
Harabu ya mali zetu,
Hushindwa kutenda kitu,

Cha kuharibu mapenzi.
485
Si kitu cha sandukuni,
Kuibwa si yamkini,
Mwivi katu haioni,
Johari yetu mapenzi.
486
Kwa kukosa pa kushika,
Mauti hutatizika,
Mapenzi kuyainika,
Kifo chetu hakiwezi.
487
Mapenzi hupenya giza,
Yakenda kwenye
Mwangaza;
Ni kitu cha kupendeza,
Kina nuru ya mwenyezi.
488
Yana ladha na heshima,
Na fahari ya daima,
Na pindi yanapohama,
Maisha hayapendezi.
489
Ni shani kwa matajiri,
Wanguvu na mashuhuri,
Na wanyonge na fakiri,
Wana kiu ya mapenzi.
490
Pendo ni kitu cha kiama,
Katika dunia nzima,
Kisha ni kitu adhama,

Mwenye pendo hapotezi.
491
Ngumu kwa dhara Johari,
Nuru yake El-kahari,
Hakishindwi kwa saburi,
Kinachoitwa mapenzi.
492
Na majangwa na mapori,
Yatishayo kwa hatari,
Hushindwa na kuhasiri,
Kizazi chake mapenzi.
493
Bahari zote za vina,
Kama huwezana kutana,
Mapenzi sitayaona,
Kuzamisha haziwezi.
494
Hushindwa na kuzamisha,
Mapenzi na kuyafisha;
Hushindwa na kudunisha,
Yakawa duni mapenzi.
495
Mapenzi kwa kila hali,
Hayawi kitu dhalili,
Wala hayana badili,
Kwa weledi wa ujuzi.
496
Kwa wenye akili nzima,
Na adabu na heshima,
Yana thamani daima,
Mapenzi hayana mwenzi.

497
Hayashindwi kwa adhama,
Ni kitu chenye uzima,
Hafiki kijapo zama,
Na milele hakiozi.
498
Mapenzi hayafi maji,
Na hushindwa wauaji,
Ni kitu cha kufariji,
Milele hufanya kazi.
499
Yana kinga ya silaha,
Hayaguswi na jeraha;
Bali mapenzi mzaha,
Mtu kusifu hawezi.
500
Hayashindiki kwa panga,
Mana kago la uganga,
Na bunduki na mizinga,
Kuyapenya kubwa kazi.
501
Hayashindiki kwa kondo,
Yana fingo la matendo,
Na pahali pa vishindo,
Huwanda yake mizizi.
502
Kwa wapenzi na watashi,
Yana kago la uishi,
Ni kitu kinachoishi,
Tuo kubwa ya majonzi.
503

Ni kituo cha mashaka,
Roho zikifadhaika,
Tuo ya kupumzika,
Taabu na nyong'onyezi.
504
Mapenzi ni jambo bora,
Kwa Imani na imara,
Bali pendo masihara,
Si kitu bali upuuzi.
505
Yana mwengo wa waridi,
Katika yangu fuadi,
Mapenzi ni zumaridi,
Ni marashi na feruzi.
506
Kwa kuwa napenda sana,
Kuitwa mshirikina,
Na ye yote sitanuna,
Siudhiki kwa mapenzi.
507
Siwi zebe kwa kununua,
Hata huitwa laana,
Mapenzi yana maana,
Hasa kwa nyakati hizi.
508
Kwa matata na kwa koto,
Maisha sasa mazito,
Mioyo ina fukuto,
Na macho yana machozi.
509
Siwi bozi kwa ghadhabu,

Hata haitwa kidhabu,
Mapenzi kwangu ,
Dhahabu,
Kuwa duni hayawezi.
510
Hata nifanywe zandiki,
Mapenzini sibanduki,
Asali mwenyewe nyuki,
Name hozi ya mapenzi.
511
Mapenzi kwangu thabiti,
Na niitwe afriti,
Ni kitu nimedhibid,
Siponyoshi hata konzi.
512
Shime wambe nimerogwa,
Na akili kuvurugwa,
Mapenzi yanapomwagwa,
Huwa yangu matembezi.
513
Kisha wambe sina macho,
Ya kuona nitendacho,
Lakini sina kificho,
Kwa kuyasifu mapenzi.
514
Kwa watu wenye busara,
Niwe haba wa fikira,
Moyoni siwi ghera,
Kuwa chini ya mapenzi.
515
Na nifanywe mutu duni,

Kwa akili na maoni,
Mapenzi mwangu moyoni,
Sibadili kwa feruzi.
516
Nifanywe sina adili,
Na mchache wa akili,
Sioni ni idhihali,
Kama ninayo mapenzi.
517
Kwa mapenzi kila mara,
Nifanywe sina imara,
haiwi kwangu hasara,
wala vigine siwazi.
518
Nisemwe kwamba mlevi,
Na fidhuli na mjuvi,
Na safihi na mgomvi,
Kileo change mapenzi.
519
Sinywi kileo cha maji,
Cha kuvuta sihitaji,
Bali napenda umbuji,
Wa adili na mapenzi.
520
Silevuki kwa vichungu,
Karaha za ulimwengu,
Nalewa fikira zangu,
Na furaha ya mapenzi.
521
Silewi pombe na mvinyo,
Kutia tumbo mifinyo,

Ni harabu ya maonyo,
Na dhana haziwi wazi.
522
Silewi mali na cheo,
Kwangu huwa si vileo,
Nalewa mapendeleo,
Na uwezo wa mapenzi.
523
Silewi nguvu na hadhi,
Ni vitu haviniridhi,
Bali nalewa faradhi,
Ya mapenziye mwenyezi.
524
Na suluhu na mwafaka,
Hulewa nikalevuka,
Hulewa nikatukuka,
Kwa hivi kuliko enzi.
525
Po pote kama hayao,
Mapenzi sina kitako,
Wale tembe pumziko,
Kama kwamba mpekuzi.
526
Kuishiwa na mapenzi,
Moyo wangu hauwezi,
Na nyinyi pia hamwezi,
Bali si wapelelezi.
527
Wachache wa tafakuri,
Tumo katika ghururi,
Imetufunga hodari,

Kila siku hutuhizi.

528
Kwa kila siku kulia,
Machozi yenda milia,
Nvuso zimefanya njia,
Na mimo ya machozi.

529
Ni mwiko kwetu kusema,
Kitu chenye kutuuma,
Si tayari kuungama,
Wala wa neno la wazi.

530
Kwa sababu roho zetu,
Ni tupu hazina kilu,
Na umaskini wetu,
Mkubwa ni wa mapenzi.

531
Tuna uchache wa utu,
Katika maisha yetu,
Kwa kupenda mno vilu,
Kuliko ndugu na wenzi.

532
Kama watu wangerukka,
Mfano wa malaikka,
Hata wakapata fika,
Chemchemi za mapenzi.

533
Watu huko wangefika,
Mambo yangebadilika,
Wote wasingalitaka,
Kuja tena nchi hizi.

534
Kuna chemchemi tamu,
Dawa yetu ya fahamu,
Na zihi ya wanadamu,
Tamthili ya pumzi.
535
Tugeomba kwa wadudi,
Mwenye kuidhi mradi,
Nchi hzi tusirudi,
Za yabisi ya mapenzi.
536
Nchi hziz za yabisi,
Watu hawana nafasi,
Wote wana wasiwasi,
La heri hawatimizi.
537
Kwa chuki kutusokota,
Nafsi zina matata,
Maneno mema huleta,
Bali hayafanyi kazi.
538
Na kinywa tukiamka,
Ni sawa na malaika,
Lakini tumechafuka,
Kwa uongo na upuuzi.
539
Ni wachache wa fadhili,
Hatuna neno la kweli,
Wala neno la adili,
Licha mbali ya mapenzi!
540

Kwa vitu kuvitapia,
Moyoni hatuna haya,
Huruma imekimbia,
Baki yetu uchokozi.

541
Kwa kupenda kugeuza,
Hapana wa kutuweza,
Kumbe twajiangamiza,
Wachache wa kumaizi!

542
Tuna mwingi kila mara,
Ufundi na usogora,
Bali hatuna busara,
Kwa upofu wa chipikizi.

543
La mbali hutusumbua,
Twaona mpaka pua,
Twaona nyingi fadhaa,
Tuchagulie mwenyezi.

544
Ya heri yamo gizani,
Twaramani hatuoni,
Maovu huja machoni,
Kwa kasi na vi kwa vikozi.

545
Twataka sana vivuli,
Visivyokuwa na mwili,
Kushikwa havikubali,
Bure tunafanya kazi.

546
Mwenyezi mungu tuwahi,

Alhamdulilahi!
Kwa kutufanya sahihi,
Njia zetu telezi.
547
Pendo kitu cha shirika,
Kwa viumbe wa kila rika,
Baraka nyingi hushuka,
Watu wakiwa wapenzi.
548
Hushuka na tuungane,
Sisi sote tupendane,
Tusiwe na tembe tone,
Mioyoni la simanzi.
549
Tupendane kila pembe,
Kila tulipo viumbe,
Na chuki isitukumbuke,
Ndani ya maangamizi.
550
Kwa kuungana fuadi,
Saburi zetu huzidi,
Tukapata la mradi,
Baraka na matumizi.
551
Kama saburi huzidi,
Maneno yangu jadidi,
Mtu hakosi zawadi,
Ya mapenzi na majazi.
552
Ni kitu chenye Baraka,
Na mambo huwa,

Mwafaka,
Halizuki la mashaka,
Wala neno la tatizi.
553
Hapazuki la matata,
Kutatiza kutafuta,
Mapenzi nyota humeta,
Hanyanyati kama mwizi.
554
Shani yake maumbile,
Kama pete na vidole,
Moyo mwenziwe milele,
Ni furaha ya mapenzi.
555
Moyo ukipenda shari,
Una taa na dosari,
Ni uchafu si fahari,
Katika zamani hizi.
556
Una mbegu ya mfundo,
Moyo ukiwa na kondo,
Na aili ya matendo,
La kweli hauhimizi.
557
Moyo ukiwa baridi,
Bahari yajitahidi,
Una faida Zaidi,
Kwa kazi na matumizi.
558
Moyo ukiwa na haya,
Mzito kushika maya,

Huwa lulu ya tabia,
Na husuni na feruzi.

559
Kwa uzuri na heshima,
Huwanda na mwili mzima,
Moyo ukiwa na wema,
Ukiwa kati ya wenzi.

560
Na huutosha kwa anasa,
Moyo wa kiyitakasa,
Hebaye kubwa kabisa,
Ua bora la mwenyezi.

561
Haushindwi roara moja,
Moyo ukiweza hoja,
Huweza pia kungoja,
Usitawi wa mapenzi.

562
Moyo mwenzie si chuki,
Mwenziwe ni urafiki,
Na taadhima na haki,
Na uhuru na mapenzi.

563
Mapenzi ni letu fungu,
Na tupendane kizungu,
Tule tamu na machungu,
Pendo letu liwe wazi.

564
Mapenzi kwetu dhahabu,
Tuwe nayo kiarabuu,
Kwa heshima na adabu,

Kama mwana na mzazi.
565
Kama hawa na adamu,
Mapenzi yetu yadumu,
Siuzote yawe tamu,
Si mapenzi ya kishenzi.
566
Tuwe nayo Kiswahili,
Mapenzi ya kuhimili,
Ya ladha kama asali,
Au kinywaji azizi.
567
Twende nayo kiungwana,
Kwa mioyo kuungana,
Mapenzi ya kufanana,
Kama pindo na tarizi.
568
Pendo tulipake rangi,
Liwe kama yungiyungi,
Lipendeze watu wengi,
Waho na beti hizi.
569
Tulipambe rangi fua,
Liwe pendo la ulua,
Na haliba ya dunia,
Liigwe na wanagenzi.
570
Tulipambe kwa manjano,
Pendo letu liwe nono,
Liwe pendo ubwa mno,
Liwe na waandamizi.

571
Kwa urembo wa manjano,
Watu wapendane mno,
Kwa lafidhi na maneno,
Katika kila makazi.
572
Kisha tupambe kwa zari,
Pendo lizidi umri,
Liwe pendo la fahari,
Liishi bila kutuzi.
573
Lichovywe na samawati,
Pendo liwe madhubuti,
Kwa watu lisaliti,
Lime kama mdizi.
574
Kwa nyota za nuuru kati,
Liwe rangi samawati,
Lionyeshe kwa umati,
Utukufu wa mwenyezi.
575
Liwe na rangi nyeusi,
Lishike zetu nafsi,
Kwa ufanifu halisi,
Kwa ambao wamaizi.
576
Lipambwe na kwa weupe,
Kupenda tusiogope,
Wenye kutupa tuwape,
Pendo bila simangizi.
577

Liwe na urujuni,
Pendo na rangi kijani,
Kila mtu atamani,
Kwa kila hali kuhozi.
578
Liwe rangi ya kijani,
Mashamba hata mjini,
Faragha na hadharani,
Na tuo za kubarizi.
579
Liwe la rangi ya fedha,
Bila waa la bughudha,
Liwe na kadha wa kadha,
Sudi na wasaidizi.
580
Liwe rangi ya dhahabu,
Lipendwe na masahibu,
Kwa mbali na wa karibu,
Wote wenye kulienzi.
581
Liwe rangi ya Johari,
Na maua ya uturi,
Kila fani ya uzuri,
Na utukufu na enzi.
582
Liwe rangi zambarau,
Bila tembe ya dharau,
Milele wasisahau,
Walipo wenye pumzi.
583
Kisha lipambwe kijivu,

Na afya njema na nguvu,
Chuki ilie kwa wivu,
Kwa kukosa mwangalizi.
584
Na tuwe nalo lisishe,
Pendo tuliimarishe,
Mpaka lituridhishe,
Kwa kutufanya wapenzi.
585
Penye nuru huwa giza,
Mwili hufa na huoza,
Mapenzi hufululiza,
Nguvu yake haituzi.
586
Jua la mchana huchwa,
Usiku wa giza hucha
Bali pendo kulificha,
Vigumu na hatuwezi.
587
Nuru za nyote huzima,
Na giza pia hukoma,
Lakini moyo hupuma,
Sikuzote kwa mapenzi.
588
Kwa pendo watu tayari,
Kwenda zuru makaburi,
Hulosha kwa kufikiri-
Kwa mtu mwenye ujuzi.
589
Hata ngambo ya kiburi,
Mapenzi yana umri,

Ndani ya moyo husiri,
Na kwa ladha hayaozi.
590
Kwa ladha na utukufu,
Mapenzi hayana ufu,
Na maishaye marefu,
Kuwa chini hayawezi.
591
Ni kitu katika dhati,
Cha dharau ya umauti,
Kwa sababu hayapati,
Natasi vya kukihizi.
592
Hushindwa na kuyadhuru,
Katika wake uhuru,
Na yameapo huduru,
Kwa heba na maangazi.
593
Ni kitu chenye thabiti,
Nguvu yote ya umauti,
Kukitisha haipati,
Kwa vita na shambulizi.
594
Kama mapenzi yaroga,
Mauti huwa na woga,
Kama huweza kupiga,
Kuyashinda hayawezi.
595
Mwendo wake hufuliza,
Bila ya kujigeuza,
Na kila mara huanza,

Hayana mwisho mapenzi.
596
Kwa kuwa kitu azizi,
Kutupwa huwa upuuzi,
Mim naona siwezi,
Nanyi pia fntaizi.
597
Kwayo nawabembeleza,
Kuinama na kuwaza,
Watu wanavyopoteza,
Majohari kwa chukizi!
598
Kwa hivi nawasihi,
Kutazama sahihi,
Neno lenye masilahi,
Kwa rai ya uchaguzi.
599
Kwa kuufanya mfupi,
Watu leo wako wapi?
Ulimwengu hauwapi,
Cho chote ila majonzi.
600
Kwa kufanya kuwa ndogo,
Duunia ina mitego,
Na wingi wa mavurugano,
Hata kuwanga huwezi.
601
Kwa kuifanya nyembamba,
Mashaka yametuwamba,
Hatuna jema la kkwamba,
Kwa misiba na majonzi.

602
Kwa kuifanya chafu,
Kwa wivu na udhalifu,
Hatuna la tahafifu,
Kila jambo hutunizi.
603
Na sisi na nchi zetu,
Hatuna miliki kitu,
Kwa sababu kila mtu,
Amehamwa na mapenzi.
604
Na ulimwengu bahili,
Wa kweli na la halali,
Hauna afadhali,
Kwetu ila pingamizi.
605
Si tayari kuridhi,
Dnia sasa kabidhi,
Ila ghera na maudhi,
Hutendwa bila ajizi.
606
Kukupa jambo zohali,
Haitendi neno hili,
Ikitaka kwako hali,
Kupinga huwa huwezi.
607
Kukupa jambo husiri,
Wala huupati kizuri,
Na milele kuhasiri,
Ndiyo yake mazoezi.
608

Si karimu wa wazuri,
Bahili kugawa heri,
Bali zawadi za shari,
Hutujia kwa mashazi.
609
Si arimu wa fadhili,
Bahili kusema kweli,
Tena ina ndimi mbili,
Wakati wa maongezi.
610
Ina umbo la kucheka,
Mfano wa malaika,
Na moyo wa kukauka,
Usio tembe mapenzi.
611
Lo lote la kukuponda,
Kwa haraka hulitenda,
Lakini la kukupenda,
Ulimwengu hauwazi.
612
Huutendwa kwa tasilihi,
Lo lote la idhilali,
Dhaifu wa kuhimili,
Wenye dhiki ya mapenzi.
613
Kukupa huwa na hamu,
Lo lote la kukusumu,
Lakini lililo tamu,
Hutoa kwa simbulizi.
614
Lo lote la kukudhuru,

Mara moja huamuru,
Bali la kukunusuru,
Kukupa we haiwezi.
615
Hutenda bila ya hofu,
Lo lote la takilifu,
Ama la kukashifu,
Bila kuwa na ajizi.
616
Nyepesi kufanya kondo,
Ama kupotoka tendo,
Kuliko kutenda pendo,
Furaha yake mwenyezi.
617
Kwa tezi wala omo,
Hakitoki kilichomo,
Na watu hugomba mumo,
Kwa kosa la maamuzi.
618
Kutwa hutungwa sharia,
Na kucha hutanguliwa,
Mfano giza na jua,
Kwa mwendo wa mageuzi.
619
Kwa bidi na kwa hoja,
Tuna wingi wa vioja,
Bali wachache wa haja,
Ya kuwa nayo mapenzi.
620
Haja yetu ya kitambo,
Huishilia na jambo,

Haja yetu ya kitambo,
Ya aushi hatuwezi!
621
Ulimwengu wa zahama,
Hauna kitu kizima,
Na litendwalo huzama,
Katu kuebuka mbizi.
622
Sikumbatii chochote,
Katika maisha yote,
Bali nataka nipate,
Buruhani ya mapenzi.
623
Pendo kwa shida sana,
Ni dhiki kuwezekana,
Mapenzi yana maana,
Kuliko ghasia hizi.
624
Hasha kwa mkono wangu,
Sitwai kuwa mwenzangu,
Chukizi ya ulimwengu,
Hata kama sina mwenzi.
625
Mapenzi ni mengi sana,
Ni shida kukosekana,
Ni nyongeza ya upana,
Na urembo nchi hizi.
626
Ni kiini cha Imani,
Na furaha ya moyoni,
Ni kitu chenye thamani,

Na milele hakiozi.
627
Ni jambo lenye sahihi,
Kisa cha nabii nuhi,
Namna alivyowahi,
Kwenda katika jahazi.
628
Wanadamu kwa wanyama,
Na wadudu wa kuuma,
Walisafiri salama,
Kwa Imani na mapenzi.
629
Simba hukudhuru,
Ng'ombe,
Nyati hukupinga pembe,
Walipatana viumbe,
Wote bila uchokozi!
630
Kondoo na mbwa mwitu,
Hawakuteta kwa kitu,
Tembo hukudhuru mtu,
Na chui hakula mbuzi!
631
Ni jambo muhimu sana,
Kujua lina maana,
Roho zikikataana,
Na Amani hatuwezi.
632
Kkwa watu wa makabila,
Huu ni mhalahala,
Kisha wajibu wa mila,

Kale na karne hizi.
633
Ni mwangaza wa kutosha,
Katika haya maisha,
Watu kujiridhisha,
Na muhimu wa mapenzi.
634
Kwa kuachia mwangaza,
Maisha twayapoteza,
Kuinama na kuwaza,
Kwa watu ni ajaizi.
635
Ulimwengu kwetu pepo,
Kama watu watakapo,
Mapenzi kila yalipo,
Kutunza na kuyaenzi.
636
Michanga yake dhahabu,
Na kazi zetu thawabu,
Wote tukiwa sahibu,
Ndani ya kila makazi.
637
Mwingi wa ladha hamu,
Na kila kitu kitamu,
Lakini hatufahamu,
Kwa uchache wa mapenzi.
638
Ni mwingi wa majohari,
Ya furaha na uzuri,
Akili na tafakuri,
Na ya hisani na enzi.

639
Kwa majohari ya dini,
Na feruzi za Imani,
Dunia si maskini,
Kwa walio na mapenzi.
640
Kwa kuwa nazo moyoni,
Lulu za matumaini,
Na furaha haihum,
Kisha haiwi tatizi.
641
kutimiza tungo yangu,
budi kuomba wenzangu,
kuniombea kwa mungu,
maisha ni utelezi.
642
Huwa pofu wamaizi,
Na wenye akili razi,
Acha mbali wanafunzi,
Wenye kujifunza kazi.
643
Huosa wenye tambuzi,
Na mabingwa wa ujuzi,
Na watu wakuurugenzi,
Sembuse ya wanagenzi.
644
Hukosa watu mahiri,
Weledi wa tafakuri,
Na hata watu hodari,
Katika kutenda kazi.
645

Hukosa wenye weledi,
Wenye akili Zaidi,
Na wenye kujitahidi,
Milele kuwa wajuzi.
646
Kisha kukosa arifu,
Wajuzi wa kusarifu,
Ya ufupi na urefu,
Na kila lisilo wazi.
647
Huukosa weledi kazi,
Nawatatuzi tatizi;
Hukosa na watambuzi,
Weledi na maamuzi.
648
Hukosa wanachuoni,
Na mafundi wa maoni,
Huanguka mashimoni,
Hata wataalamizi.
649
Ni mawindo mitegoni,
Hata adili na dini,
Na watu wenye makini,
Katika mafafanuzi.
650
Hukosa wenye fahamu,
Na walio na elimu;
Hukosa watu muhimu,
Wenye sifa ujuzi.
651
Hukosa bingwa na sui,

Hata rais wa rai,
Mambo ya dunia hii,
Mazito kwa watutuzi.
652
Hukosa wenye busara,
Watu kamange wa sera,
Kwa iumbe kila mara;
Kukosa ni ajaizi.
653
Hukosa wenye werevu,
Na watu welekevu,
Nguvu na uvumilivu,
Na saburi na ajizi.
654
Hukosa bingwa na fundi,
Watendao kwa vipindi,
Kwa nini mimi sishindwi,
Hali si fundi wa kazi!
655
Hukosa watega tambo,
Na waelewa wa mambo;
Si ila wala kombo,
Mimi kukosa utunzi.
656
Hukosa wenye fikira,
Na walewa djara,
Na weledi wa majira,
Ya miaka na miezi.
657
Hukosa wenye akili,
Mufti katika feli,

Na wajuzi wa dalili,
Falaki na kubarizi.
658
Mwanadamu kwa hakika,
Kiumbe wa kupotoka,
Wa uona mipaka,
Kuepa kosa hawezi.
659
Hali tulivyo hafifu,
Wapotofu na wachafu,
Mwenye kujua ladifu,
Rais wa wafinyanzi.
660
Na niombewe salama,
Niishi kwa kujituma,
Kuondoka na usoma
Ila siku iwe kazi.
661
Na iwe kwangu uradi,
Na daima jithadi,
Na mambo nikifanidi,
Yawe mifano ya wazi.
662
Mambo yasiwe na giza,
Yakawa tata kuwaza,
Yawe mambo ya
Mwangaza,
Faida na matumizi.
663
Tena yawe na mapimo,
Na watu kila makamo,

Wafahamu yaliyomo,
Kila kitu kwa uwazi.
664
Kisha yawe yenye utu,
Furaha kwa kila mtu
Yaridhi nafsi zetu,
Sahibu zetu wenzi.
665
Kwa faida na kwa tija,
Yawe mambo ya faraja,
Na matilaba na haja,
Ghairi ya pingamizi.
666
Yawe na wingi wa wema,
Anasa kwa kutazama,
Kila penye maongezi.
667
Ndani yawe nasi,
Madondoo ya fususi,
Yawe mambo muhtasi,
Kwa adili na mapenzi.
668
Niombewe na madua,
Ya heri na ya satua,
Maana hii dunia,
Hutatizi wang'amuzi.
669
Na nyinyi nawaombea,
Heri zote za dunia,
Kuja kwa mtawaba,
Watu wote wazihozi.

670
Wanawake wa waume,
Heri zije mzitume,
Na watoto waandame,
Kurithi wao wazazi.
671
Budi kuomba muumba,
Dunia kitu chembamba,
Na mara moja hufumba,
Japo twaiona wazi.
672
Naomba heri wapewe,
Aliyepo na ajaye,
Na wote wafunguliwe,
Hazina zenye majazi.
673
Wafunguliwe wapite,
Katika hazina zote,
Wawe radhi wasijute,
Viumbe wako wenezi!
674
Wapembeto wa umri,
Na afya kuwa urari,
Wawe na kila fahari,
Katika wako wenezi.
675
Waombao na wapate,
Na wagomvi wasitete,
Washikane watu wote,
Kwa wajibu wa mapenzi.
676

Roho na zirutubike,
Kwa mapenzi zisafika,
Na chuki ile izikwe,
Kuwa nayo hatuwezi.
677
Wape furaha ya moyo,
Kwa kupata watakayo,
Pasiwe wivu na choyo,
Wapambe kwa mapendezi!
678
Wape tunu kwa zawadi,
Na utuufu wa idi,
Na wingi wa jihadi,
Ya kuupenda mwenyezi.
679
Wenye heri ya kutenda,
Wape moyo wa kupenda,
Wawezeshe na kupanda,
Maghorofa ya ujuzi.
680
Wapambeto kwa akili,
Na kwa sudi na adili,
Na elimu mbalimbali,
Kujua na kuzihozi!
681
Kisha wafanye shujaa,
Waweze kuushambulia,
Kila ilipo fadhaa,
Na hasama na chukizi!
682
Kila mtu mwenye haja,

Ya siri na hajira,
Aandamwe na faraja,
Kwa barakazo mwenyezi!
683
Na wataka na mzuri,
Mungu usiwape shari,
Wape tabaka za heri,
Na korija za majazi.
684
Mwenyezi msaidie,
Kila akutafutae,
Siri zako aelewe,
Awe mtu mtambuzi.
685
Kila jambo lina ncha,
Nimesema sikuficha,
Kikomo hiki kuacha,
Ndiyo raha ya utenzi.
686
Utenzi wakoma hapa,
Ambao kwamba nawapa,
Kama hawatatupa,
Ndani una matumizi.
687
Beti zake kwa idadi,
Utenzi huu majidi,
Ni saba mia jadidi,
Za maua ya darizi.
688
Pambo la kila ubeti,
Ni maua rofauti,

Ya Johari na yakuti,
Almasi na feruzi.
689
Kwa wingi utawalipa,
Malipo ya kunenepa,
Wapiti wakijitapa,
Kwa nuuruze beti hizi.
690
Kumbukumbu kwa leo,
Na watu kesho wajao,
Kufanya wajibu wao,
Na kila ajizi.
691
Utakumbusha heshima,
Na matendo ya huruma,
Hupati kwa mtu wema,
Kama kuulipa huwezi.
692
Kazi hii ya thamani,
Someni shime someni,
Tena ina nuuru ndani,
Kwa walio wapekuzi.
693
Kwa watu wa mapekuzi,
Na walio na ujuzi,
Watafanya beti hizi,
Sihiri ama hirizi.
694
Someni wenye kusoma,
Utenzi huu ni mwema,
Una malipo mazima,

Na watu hawapotezi.
695
Ni kazi ya zumaridi,
Ndani inajitahidi,
Na marudi na zawadi,
Namna zile na hizi.
696
Si wa sifa wala togo,
Malenga mimi si mdogo,
Naomba penye mitego,
Mungu kunionya wazi.
697
Kama hilo hunitosha,
Katika haya maisha,
Ni lipi lisilokwisha,
Dunia na mageuzi!
698
Jina langu shaaban,
Ni mtu sina thamani,
Na kisha ni maskini,
Katika wenye pumzi.
699
Mzawa wa vibambani,
Kijiji kando ya pwani,
Si mbali tanga mjini,
Kwa mama yangu mzazi.
700
Na ni mtu si fichiki,
Afrika mashariki,
Ndiko kwetu mamluki,
Kwa kujulikana wazi.

# KIELELEZO

Adha; maudhiko

Adhama: adhimu; -enye ukubwa, -enye utukufu

Adili: sawa; haki

Aili: lawama

Aili: wenye kulaumu

Ajizi: kuchelewa

Allah: Mungu, Mola

Ambari: kitu chenye harufu nzuri, (hupatikana sana India)

Anasa: starehe; taanusi

Anga: nuru ya macho

Anga: uwazi

Apaye: mwenye kupwa

Ari: ghera;

Arifu; mwenye moyo muungwana, au mtu muhisani

Asaa: pengine

Aushi: -enye kufaulu

Azizi: -enyekupendwa, nzuri

Bahau: bahaimu; mnyama; (mtu mjinga)

Bali: lakini

Batili: isio wema;; -enye uovu/ubaya

Batini: tumbo(katika shairi, neon ‘badni’ limetumiwa kwa maana ya ‘moyo’)

Beti: vifungu vya mashairi

Bi ghairi ya: bila ya

Bia: pombe(beer)

Bumbuazi: mshangao

Buruhani: kipawa cha karama

Butaa: ushangao; mshangao

Chukizi: chukizo, machukizo, uchukizo

Daima: sikuzote

Dhaifu: enye unyonge: isiyo na nguvu

Dhalili: nyonge; dhaifu

Dibaji: utambulisho maalumu wa maandiko ya kitabu

Divai: pombe, kileo

Doria: duara, (doria ya ulinzi; mzunguko wa ulinzi yaani kwa ukuta unaolinda)

Duni; kitu kisicho thamani

El-kahari: mungu

Enzi: ‘ezi, utukufu, milki

Enzi: utukufu, ufalume

Fakiri: masikini

Falaki: unajumu; ramli; piga bao

Fani: ilimu; mambo yenye kufana; ujuzi

Faradhi: jambo la lazima, (kama chakula/mauti/ibada)

Faraja: kitulizo: (neema ya Mungu ampayo kiumbe wake)

Fauzi: ufuzo, ufaulu; ushindi

Feli zenye karaha: matendo ya kukasirisha/kuudhi

Feli: vitende; matendo

Feruzi: ferunzi, kito chenye thamani, kenye umbo la rangi ya samawati(yaani rangi ya mbingu)

Frasila: uzani wa ratili thelathini na sita(36lbs)

Fuadi. Kifua(katika shairi limetumiwa kwa maana ya moyo)

Fuadi: kifua

Fulusi: pesa; mapesa; darahima; ngwenje; fedha
Fursa: nafasi
Fursa: nafasi
Gagamizi: masingizio(gagamiza: singizia)
Ghadhabu; hasira
Ghairi ya kizuizi: bila ya kizuizi
Ghairi ya: bila ya; pasipo na.
Ghawazi: fedha; darahimu; fulusi
Ghiliba: hadaa
Ghiliba: hadaa, udanganyifu
Ghubari: wingu (maghubari: mawingue)
Gugu: nyasi; manyasi
Gulio: soko; mahali panapouziwa vitu au kununuliwa
Gumbizi: kisunzi; kizunguzungu; masuwa; masulule
Haba wafikira: mchache wa mawazo
Haba: tembe/chembe, kidogo, punje
Hahimili: hawezi kustahimili
Haigombi: haisemi: haineni
Haihuni: haikosekani;(haipotei)
Hajighasi: hajisumbui; hajipi taabu; hajishughulishi
Hakina budi: ni lazima kuwa, lazima kiwe
Halisi: hasa
Halisudi: halifaulu; halifuzu
Hapaji la viringizi: haliwezi kuja linaloviringa/linalosumbua
Hari: joto
Hatuhizi: hatulaani; hatulani; hatuapizi
Hautangi: haufazaiki; hauwayiwayi; haubabaiki
Hauvizi: hauharibu(hauharibiki)
Hawa: hawaa; matamanio ya moyo
Hawamudu: hawajui; hawajijui
Hawangi: hawezi kuhesabu; hawezi kutazama

Hawawazi: hawana mawazo bora
Hawazi: hafikiri
Hayanyati: hayashiki(kama gamu)
Heba: haiba; umbo jemausahiba: urafiki
Hiba: hidaya, tunu
Hila: ujanja
Hima: upesi, haraka
Hindi: india; uhindini
Hosha: siwezi; haiwezekani kabisa
Hubarizi: hulizungumzi
Hububu: tembe(kama ya mchele au mtama nk) chembe
Huduru: huzunguka
Hugomba mumo; husema humo humo
Hukinai: hutosheka
Husiri: huendelea
Husiri; huchelewa, hakawilia; hulimatia
Huta hapewa dhahabu: japo nikapewa dhahabu
Huwayawaya: hubabaika; huhangaika; hutangatanga
Idhilali: unyonge
Ikisadifu: ikikabili
Ikome: iishe, imalizike; iishie; isiendelee
Inatukanganya: inatubagua; inatutenganisha
Ingalituchusha: ingalituchokesha, ingetuchokesha
Jadi: asili, (Kiarabu ni 'babu' mzaa baba au mama)
Jaha: utukufu
Jaha: utukufu
Jahili: mjinga, mpumbavu, juha
Jazila: uzani wa ratili 434(yaani pishi 62)
Jinamiu: shetani mwovu
Jitimai: huzuni; majonzi; simanzi
Johari; kito; jiwe la thamani

Josho: kujiosha

Joyo: moyo mkubwa; mtima mkuu, (usiokubali maongozi)

Juma: ijumaa

Kago: fungo la madawa ya uchawi

Kalamzi: udanganyifu; hadaa

Kamange wa sera: watu wastadi;

Kangara: jina la pombe/tembo: kileo

Kani: bidii; juhudi au nguvu

Kanzi : hazina

Karaha: makuruhu; tendo lisilopendeza

Kasumba: bangi

Katu kuebuka mbizi: haiwezekani kabisa kuzuka, yaani kutokezea nje

Kero: maudhi; maudhiko

Kila kadiri: kila kipimo

Kilizi: kilio

Kitimbi: jambo la fitina

Kitunga: chamba; kitone cheupe kilichoingia katika mboni ya jicho

Kiwango: kikomo; kiasi; kadiri; kipimo

Kiwi: kiowu; lakini neon hili ‘kiwi’ katika shairi neon ‘giza’

Kondo: bangu; vita; kitali; adharusi

Kondo: bangu; vita; kitali; ngondo

Konyaki: konyako; (jina la tumbaku wanayoitumia wajaluo)

Konzi: punje; tembe, kama vile yam tama au mchele

Korija: ishirini; vitu ishirini kwa pamoja

Kuawakali: kuanza tawakali=anza

Kudhili: kutesa, kudhalilisha(dhalili: enye unyonge)

Kudokoa: kumenya; kunyotoa; kumega, kwambuwa

Kudurusi: kusoma kwa makini zaidi zaidi

Kufariji: kurehemu; kusahilisha; kuneemesha

Kufuru: dhambi; madhambi
Kughilibu: kuhadaa
Kuhama: kutama, kugura
Kuhizika: kulaanika
Kujitambu: kujibidiisha
Kukashfu: kutangaza aibu, au kueleza lenye aibu, kuumbua
Kukidhia: kutoshea
Kukihizi: kukifedhehi, kukiabisha
Kukusumu: kukuua
Kulienzi: kulitukuza
Kumaizi: kufahamu
Kunenepa: kuwanda, kunona
Kunitoweka: kunipotea(Kutoweka, kupotea)
Kununa: kukasirika; kughadhabika; (kuwa na uso wa hasira)
Kunuti: omba dua kwa Mungu
Kupambanua: kuchangua; kuweka mbali mbali
Kuratibu: kuandika
Kushanfu: kuheshimu, kuchukuza
Kutanguwa: kuweka mbali mbali
Kutimu: kutimia, kukamilika
Kutoweka: kupotea
Kutuhizi: kutufedhehesha
Kutukebehi: kutuaziri; kututolea siri zetu nje
Kutunzwa: kulindwa, kuangaliwa vema, kuchungwa
Kutuzi: harufu inayonukia vibaya
Kutuzi: harufu mbaya; kikwapa
Kuwanga; kuhesabu, au kutazama
Kuyaenzi: kuyatukuza
Kuyafisha: kuyaua
Kuyahami: kuyahifadhi, kuyachunga, kuyalinda
Kuzi: kasiki; balasi; nzio

Kuzingatia: kufikiria mawazo bora

Kuzirai: kuzimia(kuzisihi; kuzibembeleza)

Kwa sera: kwa njia

Kwa tasihili: kwa mara moja; kwa upesi sana

Kwa tezi wala kwa omo: kwa nyuma wala kwa mbele

Kwa watu nizo kwa mzo: kwa wanaopimiana mambo kwa usawa

Labda; labuda, pengine

Lafidhi: matamko; matamshi

Laity: lau kuwa

Latifu: Mungu mpole

Libasi: nguo, kivao; kivazi

Licha: wacha, achilia

Limetakadamu: limeanza, limetanguha

Lingefanya majilio: lingefanya kuja; lau lingekuja

Lisitaiti: lisibane; lisikaze; lisikabe

Litalazimu: litalazimika, itakuwa ni lazima

Litatiririka: litachuruzika

Lubu: kiini cha jambo, au asili ya kitu

Maamuma: mfuasi; wafuasi

Mabuma: mabumu; mabundi: (jina la ndege anaeitwa babae watoto)

Madhila: mashaka; mateso; idhilali

Madufu: wasio thamani

Maghibu: pepo za tufani; upepo wa kimbunga

Magunge na wanagenzi: mabingwa na wanafunzi

Mahabubu: -enye kupendwa

Mahasusi: -lokusudiwa

Mahiri; -enye akili bora, -enye maarifa; -enye akili timamu

Maize: mwenye akili bora, mwenye fahamu nzuri

Majazi: vipawa; kipawa cha maongezeko

Majazi: vipowa: vipewa; vipao

Majonzi: huzuni; masikitiko

Makala: maelezo, mazungumzo, maneno

Malau: malambi; makombo; masazo ya chakula

Maliki: mfalme; mfaume

Maliki: mfalume; mfaume, mfalme

Mana kago; yana fungo la kujikinga ili yasifikwe na madawa ya wachawi kwa urogaji

Mansubu: misiba

Manukato: mafuta yanayonukia harufu nzuri/njema

Maono: maoni, mawazo, fikira yenye busara

Maonyo: mafunzo

Mapenzi ya maki: mapenzi yenye nguvu.(maki=unene)

Maradufu: mara mbili

Mashazi mashazi: matopa matopa; kwa wingi sana mno

Mashazi: utungo wa vitu pamoja, kama vile samaki au makanju

Masihara: dhihaka

Masogora: wakuu wa wapigaji ngoma; (viongozi wa ngoma)

Masukuba: marafiki; wendani; mbasi

Matilaba: maombi

Mawazo: fikira

Mdakuzi: mchunguaji wa siri za watu

Mdizi: mgomba

Mfawidha: cha kuchosha

Mguno: kitunu, (yaani kusema “Mh”)

Mhalahala: wasia; onyo

Miali: miangaza

Mie: mimi

Mifinyo; maumivu

Mifuo: kandono mwa bahari/kando ya bahari

Milia: mistari; misitari

Milki: mali

Miski: kitu chenye harufu njema

Mizimu: mahali ambapo wachawi huwalingana mashetani

Mizuka: mashetani

Mizungu: kinyume; hiyana; uhaini

Mjarabu: enye kujaribu

Mjeledi: kiboko cha kupigia

Mkazi: mkaaji wan chi au mji fulani

Mkondo: njia ipitayo maji

Mkuku: utako wa jahazi/merikebu au mashua

Mmsga: uhai

Mpotovu;-siyo nyooka

Mtaizi: mtakataa, yaani mtaiza

Mtengwa: mtu alietengwa; alieekwa kando

Mtenzi: mtendi; mtendaji

Mtindi: pombe, kileo

Mufti; mtaalamu mkuu

Musri: nchi ya Egypt

Mvi: nywele nyeupe

Mwanagemi: mwanafunzi; mtu anayefundishwa jambo; mwari

Mwenyezi: Mungu mwenye enzi

Mwenzi: mwenzi wake; mwenzake; mwenziwe

Mwieni radhi: msameheni; niweleyani radhi

Mwiko: miko; ‘kambe, (mambo unayojizuia kutenda)

Mzo: uzani wa ratili 350-60

Na ambao kwamba asi: na ambao wameacha/wamehuzi/mefanya uasi

Na tuo za kubarizi: baraza za mazungumzo

Na watatuzi latizi: na waondoao matatizo

Nahau: ufasaha

Nakidi: pesa, darahima; fedha; ngwenje

Nakisi: nadhani; nafikiria lakini sina hakika

Nano; lililinona; zuri; jema

Nasaha: maonyo mema; mafunzo mazuri

Nashuku: nadhani, ninadhani, nafikiria

Nasi: msingi mwema: shabaha nzuri

Natatizika: ninatatizika, ninapata tabu

Natumai: naamini

Nawaza: nafikiri

Ndaniye: ndani yake

Ngoa: matamanio

Ni ajaizi: ni kazi yake; ni desturi yake

Nifululize: nifulize, niendelee zaidi

Nikifanidi: nikifaidi, nikipata faida

Nilikazana: nilijibidiisha, nilifanya bidii, nilifanya juhudi,

Nimepeleleza: nimetazama kwa makini, au nimechungua kwa makini sana

Ningeizi: ningalikataa; ningeiza

Ningeslahabu: ningependa, ningeipenda

Nisikwae: nisikunguwae, nisijikwae

Nitaajizika; nitachelewa

Nitanena: nitasema; ‘taamba

Njozi: ndoto; ruwia

Njozi: ndotu; ruwia

Nondo: jina la nyoka mkubwa sana anayeweza kumeza ng’ombe mzima au watu kadhaa

Nyamafu: nyama yam fu; mnyama aliekufa; mzoga

Nyenzo: miendo; nyenendo

Nyerezi: utaratibu; polepole

Nyong’onyezi: -enye kuufanya mwili kuwa mlegevu

Nzima: kamilifu, ilokamilika

Pindi: muda

Pingamizi: pingamano, upinzani, (enye kupinga)

Pingamizi: upinzani; pingo

Pitu na pituzi: tabu na mashaka; hasara na taabu

Punje: chembe; kidogo

Pupa: fazaa

Rabsha: ghasia; fujo; mayowe; kelele

Rabsha: kelele; ghasia; yungu wadhi

Rai: maono; maoni

Razi: razini; iliyokamilika; enye uwekevu

Sahuri: subira ; ungojevu

Sakara: ulevi; kileo

Salihi: -enye wema

Samawati: rangi ya mbingu

Sanaa: uundaji; muundo

Sayari: nyota

Shahamu: mafuta ya mfupani

Shambulizi: shambulio(Mashambulizi; mashambulio)

Shani: ajabu; ibra; tendo la kuajabisha

Shime: bidii

Shwari: hali ya utulivu

Si kwamba: si kuwa

Si tayari: siko tayari, sijawa tayari, si kuwa tayari, sitakuwa tayari,

Si wazi: zimejificha(Siwazi=sifikiri)

Si yamkini: haiwezekani

Sifaze: sifazake

Sijakoma: sijafika mwisho; sijaisha

Silevuki: silewi; silevywi; siwezi kuleweshwa na pombe

Silika: tabia, sifa, ,wendo

Simangizi: usutano; msutano; usuto

Simanzi: huzuni: jitimai; sikitiko

Sudi: suudi, ufaulu; (bahati njema)

Suwest: chuma;(yaani chuma cha suwes)

Ta'bu: taabu

Taabani: hoi; enyekuchoka

Taanisa: starehe

Tadhuriwa: nitadhuriwa

Tahafifu; sahali

Takilifu: ta'bu, taabu, dhiki

Tala na simanzi: taabu na huzuni

Tambuu; akili inayotambua mengi

Tamthili: mifano, methali

Tanga: guo linalofungwa katika mlingoti wa chombo kama vile jahazi au mashua

Tarakimu: hesabu; idadi

Tarizi: mshono

Tatizi: matatizo tata

Tauni: ugonjwa unaotokana na panya

Tawapa: nitawapa

Tijara: faida

Tijara: faida; tija; na tija

Toadhima: utukufu

Tuhuma: dhana mbaya; kufikiria viovu; shaka

Tuhuma: shaka; dhana

Tumbuizi: tumbuizo, uimbaji, mtumbuizi=muimbaji; tumbuizi=nyimbo za kuliwaza

Tuna tata na tatizi: tuna taabu na matatizo

Turufu: jambo maalumu

Ubazazi: udanganyifu

Ufu: kifo, (siku ya ufu=siku ya kifo/mauti)

Uhasimu: utesi, ugomvi
Ujasiri: ushujaa
Ukiwa: upweke; uyatima
Ukufi: usawa
Ulaghai: udanganyifu
Ulua:cheo; heshima
Uluwa: cheo; heshima
Uma: watu(umma)
Umati: halaiki; watu wengi, umma
Umbuji: uhodari wa kusema/usemaji
Umeazimu: umeazimia, umekusudia
Uokovu: uokozi
Upzi: upuuzi, au jambo lisilokuwa na faida wala maana yoyote
Uradi: tendo la siku zote unalotumia kama dsturi au ada yako
Urujuuni:rangi nyekundu kama vile damu
Utakaso: utakatifu; unadhifu; usafi
Utaratibu: upole
Utashi: uhitaji; utahaji
Utovu: ukosefu
Utovu: ukosefu, ukosaji
Utu: uungwana; (yaani) matendo bora
Utungo: ushairi
Uturi: uzuri; (kiarabu "Utri" ni mafuta yanayonukia harufu njema/nzuri)
Utuvu: kituo, makini, utulivu; kutokuwa na hangaiko
Vikozi: vikundi
Wa tafakuri: wenye kufikiria mambo mema
Waa la bughudha: doa la utesi, au la hasama
Waadilifu: watendao haki
Wabezi: wenye kudharau; wanaodharau
Wachopozi: watopozi; wenye kutopoa

Wadudi: Mungu
Wahabu: Mungu
Wahedi: moja
Wakajihisi: wakajiona: wakajifikiria
Wakazi: wakaaji, (wanaoishi katika nchi)
Wakosoe: watoe makosa, wondoe makosa, wasahihishe
Walichokifyosa: walichokidharau
Wamaizi: waelewa, wafahamu vema
Wamba: wasema; wanasema; wanena
Wanagenzi: wari; wanafunzi
Wari: wanafunzi wa mambo fulani
Wataalamizi: wenye kufunza elimu
Watahozi: watapata
Watakariri: watarudia mara kwa mara
Watakithiri: watazidi
Watatuzi: wenye kutatua; wenye kuondoa matata
Watawa: wachaji Mungu
Watunga: watungaji, washairi
Welewa: wenye kuelewa
Wenezi: uwenezi(wa Mungu utukufu)
Wenginewe: watu wengine
Yana fingo: yana hirizi ya uchawi
Yanapohoma: yanapogura; yanapoondoka
Yatabarizi: yatazungumzwa
Yatajizika: yatajifukia
Yatanihizi: yataniaziri
Yawambe: yemee; yaote
Yungiyungi; aina ya maua yanayomea katika maji ya ziwa
Zahama: ghasia; kishino
Zana: silaha za vita
Zarambo: pombe, kileo

Zari: nyuzi za rangi ya dhahabu au fedha

Zebe: mjinga; jura; mpumbavu; zuzu; bunga; jahili; juha; pumbe

Zihi: nguvu; afya

Zimegura: zimehama; zimeondoka; haziko kamwe

Zisihulu: zisiishe, zisikome; zisimalizike

Zohali: kisirani: pingamizi

Zohali: nuhusi, kisirani

Zumaridi: kito kama vile almasi